**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni | Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |

| | |
|---|---|
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Omar Ali Shehe | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Abass Juma Muhunzi | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 46.Mhe. Ali Moh’d Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 57.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 58.Mhe. Hasnuu Moh’d Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 59.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 63.Mhe. Moh’d Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 64.Mhe. Mustafa Moh’d Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 67.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |

| | |
|---|---|
| 69.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 70.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 71.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 73.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |
| 76.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake. |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**.

**Kikao cha Pili – Tarehe 22 Januari, 2009**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Mwenyekiti,(Mhe. Ali Mzee Ali) Alisoma Dua.*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 39**

**Sheria ya Kudhibiti UKIMWI**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu)** - Aliuliza:-

Kwa kuwa maambukizo ya virusi vya UKIMWI hayaonyeshi kupunguwa na maradhi ya UKIMWI yanaongezeka siku baada ya siku.

Je serikali ina mpango gani wa kuanzisha sheria ya kudhibiti UKIMWI na maambukizi ya UKIMWI na hasa kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano tayari limeshapitisha sheria hiyo, na kwa sababu sheria hiyo inatumika upande mmoja tu wa Jamhuri ya Muungano.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika asubuhi hii kufika kwenye kikao tukiwa wazima kabisa na wenye afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa ruhusa yako naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Tume ya UKIMWI imeanza maandalizi ya sheria ya kudhibiti UKIMWI hapa Zanzibar. Mawasiliano ya awali yamefanywa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kuhakikisha ushiriki wao kikamilifu katika maandalizi hayo. Washirika wa Maendeleo wameahidi kutupatia mtaalamu ambaye atafanya kazi kwa kushirikiana na wataalamu wa ndani. Hadudi rejea kwa ajili ya kazi hiyo zimeandaliwa na tunatarajia kazi itaanza wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, sheria itagusa maeneo mbali mbali ya sera ambayo utekelezaji wake utahitaji nguvu ya kisheria, ikiwemo suala la kuambukiza kwa makusudi. Tunategemea kwamba sheria hiyo itakapokuwa tayari itajenga mazingira mazuri ya kupambana na UKIMWI na itasaidia katika kuhakikisha haki za binaadamu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI zinalindwa na pia kuheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tayari sera ya kudhibiti UKIMWI imepitishwa na Baraza lako tukufu katika kikao chake cha mwezi wa Oktoba, 2006 ambayo inahitaji nguvu ya kisheria

katika utekelezaji wake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, maradhi haya ambayo ni maambukizo ya UKIMWI yamo katika maeneo mbali mbali katika nchi yetu. Baadhi ya watu ambao wanajulikana hasa kuwa wana maradhi haya huwa wanaingiliana na watu ambao hawana UKIMWI bila ya kuwatambua. Kwa kuwa sheria hiyo ni muhimu sana kuletwa haraka ili kuinusuru jamii yetu ambayo haijaambukizwa na maradhi hayo ili ipate manusura.

Je, pamoja na juhudi ambazo zinaendelea hivi sasa, Mhe. Waziri atatoa wito gani kwa watu wenye tabia kama hiyo, ambao wanajijua wana virusi vya UKIMWI na wakawaambukiza watu wengine ambao hawawajui.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, bado hatujapata uthibitisho wa kwamba kuna watu ambao wenye virusi vya UKIMWI wakawa wanawaambukiza kwa makusudi, yaani wanawaingilia watu wengine kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yetu kitu ambacho inakiomba ni kwamba watu kwanza waachane na zinaa, hilo ndio la mwanzo. Kwa sababu hata kama mtu ameambukizwa na virusi vya UKIMWI kama hukufanya naye tendo la zinaa bado hana sababu ya kuweza kukuambukiza virusi hivyo vya UKIMWI.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tunasisitiza kwamba wale ambao waliokuwa tayari wameshaamua kupotoka basi watumie kinga. Kwa sababu kama dhambi kutumia kinga, basi hata hilo tendo lenyewe vile vile ni dhambi. Sasa sitaki kutumia ule msemo wa kusema kwamba ”ukila nguruwe kula aliyenona” kidogo nitakuwa ninakosea. Lakini ni vizuri ikiwa umeamua kupotoka na kumuasi Mwenyezi Mungu, basi bora upotoke kweli kweli yaani vaa kondom zako halafu fanya maovu yako.

Lakini kimsingi kitu ambacho ninakiomba ni kwamba watu wasikubali kufanya mapenzi na mtu ambaye hajafunga naye ndoa na wala asikubaliane naye kimapenzi. Kwa sababu vinginevyo ndio itakuwa unaikaribia zina na matokeo yake inaweza ikaja ikampata mtu ambaye hakukusudiwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kitu ninachokiomba ni kwamba sasa hivi usimuamini mtu hata ukimuona anang’ara kiasi gani. Kwa sababu siku hizi kuna dawa za kurefusha maisha ambazo zinampa mtu nguvu mpya na ari mpya ya kuweza kufanya kazi zaidi. Kwa hivyo, kitu ambacho ninakisisitiza ni kuwa bado watu waepukane na mambo ya zinaa, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Moh’d Ali Salim:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili tunaambiwa kuwa maambukizi yanaongezeka siku hadi siku.

(a) Kwanza naomba nijuwe je, habari hii ni kweli?

(b) Kama ni kweli imejulikanaje kama ni kweli?

Kwa sababu inawezekana hao wanaogunduliwa wapya si wapya ni wakongwe wameanza zamani. Je, kuna njia gani ambayo wizara itafanya ya kujua katika Zanzibar kuna watu wangapi wenye virusi vya UKIMWI, ili baadae waje wapime tena waone kuwa kuna ongezeko au hakuna ongezeko, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, suala la maambukizo ya UKIMWI katika takwimu za hivi karibuni bado zinaonesha kwamba Zanzibar tumejitahidi sana kudhibiti maambukizo. Maambukizo yetu hayajavuka kiwango cha asilimia 0.6. Kwa hivyo, bado tunashukuru sana wananchi wetu na tunawaomba waendelee na tabia nzuri za kuweza kujilinda, hasa katika hivi vishawishi ambavyo vinachochea maambukizi ya UKIMWI.

Samahani Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Moh'd Ali Salim arejee swali lake jengine amekusudia kitu gani, maana limenitoka kidogo.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni kuwa hivi sasa hawaeleweki ni watu wangapi Zanzibar nzima waliokuwa na UKIMWI. Je, tunasema UKIMWI unaongezeka ni kipimo gani tulichotumia kuona kuwa UKIMWI unaongezeka?

Je, serikali ina mpango gani wa kuwajua watu wote waliokuwa na UKIMWI, ili baadae tukisema unaongezeka tujuwe kuwa kweli umeongezeka?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, suala la kuongezeka kama nilivyosema kuwa bado maongezeko ya UKIMWI sio makubwa. Kimsingi kwa kuwa bado watu wanaendelea kwenda kupima na wanagundulikana watu wapya, ndio maana tukawa tunasema kwamba maambukizo ya UKIMWI bado yapo yanaendelea.

Suala la kuwa ni kigezo gani tunachochukua cha kuweza kujua kuwa haya ni maambukizi mapya na sio yale ya zamani. Kwa kuwa sasa hivi tunaandaa hiyo sheria, mimi nafikiri baadae mswada utakuja hapa. Kwa hivyo, tutakapokuwa tunachangia, basi tutaweza na sisi vile vile kuingiza mawazo yetu katika kuiboresha hii sheria ambayo tutakayoweza kuiunda.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria hizi za haki za binadamu ambazo hatutakiwi kumlazimisha mtu kupima kwa lazima. Sasa hivi labda watu ambao wanaopimwa kwa lazima ni wanawake waliokuwa wajawazito na wanapimwa kwa sababu moja tu, kwamba wale madaktari wanapowashughulikia, basi na wao wawe na usalama zaidi, wasije wakamshughulikia mgonjwa matokeo yake na wao wakajawakapata maambukizi.

Vile vile wajawazito wanapopimwa virusi vya UKIMWI inaangaliwa pia kama mama ameambukizwa, ili madaktari waweze kukilinda kile kizazi kitakachozaliwa kisipate yale

maambukizi, ndio maana kinamama wajawazito wakawa wanapimwa kwa lazima. Mpaka sasa hivi sheria hizi za haki za binadamu bado hazituruhusu kuwalazimisha watu kuwapima kwa lazima.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Zanzibar tunavyovitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi na pengine si muda mrefu kutakuja na vitambulisho vya kitaifa, yaani vya Tanzania nzima. Kama Baraza letu litakuja kutengeneza sheria ambayo italazimisha watu wote wapimwe ili wajulikane raia fulani mwenye kitambulisho namba fulani huyu tayari ameshapimwa, au kama hajapimwa akija akipimwa tena yataonekana sio maambukizo mapya pengine alikuwa nayo zamani.

Lakini haya mambo yote inabidi sisi wenyewe hapa Barazani ndio tunatunga sheria, itabidi tunapochangia ule mswada, basi tujaribu kuingiza yale mawazo yetu, tukiona kwamba Baraza limeridhia kwamba watu wapimwe wote, tutaangalia na hizo sheria za haki za binadamu basi tunaweza tukafanya hivyo, ili kuweza kujua kwamba kuna maambukizo mapya au wale waliokuwanayo ndio wale wale wa zamani, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Namshukuru sana Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kwa majibu yake mazuri sana, lakini na mimi napenda kutoa ufafanuzi wa ziada kwa suala la nyongeza la Mhe. Moh’d Ali Salim.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba taarifa za UKIMWI zinaonesha kwamba kuna maambukizo mapya yaliyotokea kila mwaka, pamoja na kwamba unapofanya mahesabu ya haraka haraka, wataalamu wanatuambia kiwango cha maambukizi kiko 0.6, lakini hili halithibitishi kwamba hakuna ongezeko, kwa nini?

Sisi tunajua kwamba utaratibu tunaoutumia sasa kupata hizi takwimu ni kwa watu ambao wanakwenda katika vituo vya afya kwa sababu mbali mbali. Wapo wanaojisikia pengine wana maradhi ambayo yanachukua muda mrefu sana kila akipata tiba anaona mhh! Mbona kama kuna vitu katika mwili wangu si vya kawaida, kwa hivyo wanakwenda hospitali kwa sababu maalum. Kwa maana hiyo wanapokwenda kwenye vituo vya afya ndio wanapimwa.

Kwa hivyo, inawezekana na hivyo ndivyo ilivyo, kutokana na sababu ambazo zinachangia maambukizi ya ukimwi, maana kubwa kwa asilimia 80 ni zinaa na ni vitu ambavyo vinafanyika kwa siri sana. Sasa kuna uwezekano mkubwa sana, kuwa kuna idadi ya watu kubwa sana ambayo kwa macho ya kawaida hatuioni wapo, inawezekana hivyo.

Sasa utaratibu ambao unatumiwa na serikali katika kupata taarifa zaidi, moja ni hilo kuwapima watu ambao wanakwenda kwenye vituo vya afya. Lakini la pili, katika vituo vyetu vya afya na *clinic* mbali mbali hapa Zanzibar, hivi sasa kuna huduma mbali mbali za kupima. Vipo vituo vya hiyari ambavyo viko nje ya utaratibu wa vituo vya serikali, kazi yake navyo ni kupima watu, ili kujua afya zao. Lakini kwa bahati mbaya utaratibu

tulionao haujatufikisha mahali kwamba sasa tumlazimishe kila mtu, uanze sasa kuchukua polisi na uhakikishe unakwenda kwenye kila nyumba. Utaratibu huu kwa mujibu wa sheria za haki za binadamu si utaratibu mzuri sana. Tunaendelea kuwaelimisha wananchi kwamba wajitokeze kwa hiyari.

Kwa nini wananchi wajitokeze kwa hiari, kuna faida gani? Faida iliyopo ni kwamba sasa ziko huduma za dawa za kurefusha maisha, iwapo atapimwa mtu na kwa bahati mbaya ataonekana kwamba ana virusi vya UKIMWI, atakuwa chini ya uangalizi wa madaktari wataangalia kiasi cha uwezo wake huo wa kuhimili dawa nakadhalika. Sasa pale ambapo kiwango chake cha afya yake pengine kitaruhusu matumizi hayo ya dawa, wataalamu wanaweza kumpatia hizo dawa kama bado, wataendelea kumuangalia mpaka pale watapohisi kuwa sasa tayari wamuanzishe kutumia hizo dawa, hilo moja.

Lakini kwa wale ambao pengine hawajapata maambukizo ya virusi vya UKIMWI, lakini pengine tu kutokana na namna ya maisha yao walikuwa na wasi wasi na kusema mhh! Kwa utaratibu wangu wa maisha haya nina wasi wasi. Lakini mbona ninaishi kwa wasi wasi, sijui ninao au sijui sina. Sasa unapokwenda kwenye kituo cha afya inapatikana faida, kwa sababu sasa wataalamu watakuthibitishia kwamba wewe uko salama.

Lakini ukishakuwa salama, basi sasa ubadilishe utaratibu wako wa maisha. Kwa mujibu wa maadili ya dini ya Kiislamu. Kwa maadili ya kisayansi, afya za tiba na kadhalika, wanasema njia iliyosahihi zaidi katika maisha ya binadamu kumkinga mtu na virusi vya UKIMWI mpaka sasa njia pekee ni ile ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi ameisema ya zinaa.

Vitabu vyetu sisi tunaofuata kitabu cha Kurani tukufu kinatueleza hivyo, na mafunzo ya Kiislamu yanaeleza hivyo na wale wanaotumia biblia nao inaeleza hivyo. Kwa hivyo, tukifanya ujanja ujanja haitatusaidia sana. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, maadhimisho ya siku ya UKIMWI kwa mwaka uliopita yaliambatana na maonesho ya mavazi, ambayo kidogo yalikuwa yanafanana na mashindano ya ma-*miss*.

Sasa swali langu liko hapa. Je, pamoja na kutungwa sheria hii kwa kupitia Afisi yako Mhe. Waziri Kiongozi, ina mpango gani wa kudhibiti mporomoko huu wa maadili vikiwemo vivazi ambavyo si vya heshima.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa Zanzibar hakuna sheria iliyopiga marufuku mashindano ya mavazi, lakini naona hatujaandaa utaratibu wa kuyaruhusu vile vile haya mashindano ya mavazi. Hata Mhe. Waziri Kiongozi hapa hapa Barazani aliwahi kulizungumzia sana, na akasema kwamba wanawake wa Zanzibar wote ni wazuri, tena wazuri kweli kweli. Kwa hivyo, ile mambo ya kwenda kujionesha sijui uvae nini. Ah! Unamuonesha nani na wewe tayari ni mzuri.

Kwa hivyo, hili suala la maonesho ya mavazi sina uhakika kama limewahi kufanyika katika haya maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani. Kwa kuwa suala hili liko chini ya wizara yangu, basi kama limefanyika basi tunaomba radhi sana. Pengine limefanyika bila ya kushirikishwa moja kwa moja wizara yetu.

Vile vile waheshimiwa tunaomba kwamba msije mkasubiri kutuuliza maswali tu, mnapoona kuna mmong'onyoko wa maadili unafanyika, basi sisi tuambieni pale pale, mitandao sasa hivi iko wazi, tuna uwezo wa kutumia vyombo vyetu kudhibiti hii hali ili isipotoke.

Nadhani Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nafikiri kama hivi, ameshaombwa ombwa sana kuhusu matamasha ya mavazi na amekuwa akiyakataa sana. Bado sisi kwa mila zetu na silka za Wazanzibari kwa mashindano ya mavazi tunavyoyaona, sisi kwetu hatuoni kuwa ni mambo ya maana, zaidi ni kuwapotosha watoto wetu. Kwa hivyo, wale ambao utamaduni wao unawaruhusu, basi wale wacha waendelee. Lakini kwa Zanzibar sisi bado tunahisi mwanamke akivaa kanzu yake na mtandio akijitanda vizuri, tunaona yule ndio tayari yuko katika mashindano. Huko barabarani basi anakuwa tayari ameshashinda, hatuna haja ya kwenda kumuanika hadharani.

**Nam. 10**

**Ukosefu wa Kifaa cha "Callobration Can" Katika Vituo vya Mafuta vya Zanzibar**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Ali Abdalla Ali)** – Aliuliza:-

Mapato yanayopatikana katika biashara ya mafuta ya Taa, Petroli na Diseli husaidia sana uchumi wa Zanzibar ingawaje kwa muda mrefu sasa kumekuwa na tatizo la ukosefu wa kifaa cha kupimia mafuta hayo kiitwacho "Callobration can" ambacho hukodiwa kutoka Tanzania Bara kila kinapohitajika.

(a) Kwa kuwa kifaa hicho ni muhimu sana, kwa nini wizara haisimamii ununuzi wa kifaa hicho.

(b) Je, wizara haioni kuwa kukodi kifaa hicho husababisha hasara kubwa kwa serikali.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 10 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane naye kwamba kwa muda mrefu kifaa cha ukaguzi wa mafuta yaani *'check pump'* hakikuwepo hapa Zanzibar. Lakini naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kuwa kifaa hicho kimeshanunuliwa na kimeanza kutumika katika shughuli za ukaguzi wa mafuta.

**Nam. 49**

**Utatuzi wa Migogoro Kazini**

**Mhe. Anaclet Thobias Makungila** – Aliuliza:-

Miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni kuendelea na ukaguzi sehemu za kazi na kusimamia utekelezaji wa sera ya ajira na sheria za kazi.

(a) Je, ni migogoro mingapi iliyotatuliwa sehemu za kazi kuanzia 2003 – 2008 na ni sekta ipi inayoongoza kwa migogoro kazini.

(b) Ni sekta ipi inayoongoza kwa uvunjaji wa sheria za kazi.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 49 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu kati ya mwaka 2003 – 2008 imepokea migogoro au malalamiko ya kazi 600 kati ya hiyo 522 ilipatiwa ufumbuzi na Wizara yangu kama nitakavyoeleza hapa ndio namna ya migogoro ilivyoshughulikiwa.

| MWAKA | MIGOGORO ILIYOPOKELEWA | MIGOGORO ILIYOSULUHISHWA |
|---|---|---|
| 2003/2004 | 105 | 90 |
| 2004/2005 | 212 | 180 |
| 2005/2006 | 121 | 113 |
| 2006/2007 | 83 | 71 |
| 2007/2008 | 79 | 68 |
| JUMLA | 600 | 522 |

Aidha, takwimu zetu zinaonesha kwamba wenye kuongoza kwa migogoro ni taasisi za hoteli na ujenzi.

(b) Tokea kuanza kutumika Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005 ambapo Sekta ya Umma na binafsi zinashughulikiwa na wizara yangu, sekta ya binafsi bado inaongoza kwa kutotimiza masharti ya Sheria za Kazi.

Aidha, matatizo hutokea katika kazi za hoteli na kazi za ujenzi. Hata hivyo, wizara yangu inaendelea kushirikiana na wadau wa masuala ya kazi ili kuiimarisha sekta hii na kuondokana au kupunguza matatizo yasiyo ya lazima kutokea sehemu za kazi. Ahsante.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa asubuhi ya leo kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda nimuulize Mhe. Waziri, kwa kuwa katika jibu lake alitaja migogoro iliyosuluhishwa na ile iliyokuwa haikusuluhishwa.

a) Je, ile migogoro iliyokuwa haikusuluhishwa inaendelezwa au ndio inaachwa kama ilivyo.

b) Kwa kuwa migogoro hii ni mingi. Je, chanzo chake hasa ni nini, ni kule kazini au ni wizara yake inakuwa haina mkataba maalum baina ya mfanyakazi na wale waajiri. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumfahamisha Mhe. Rashid Seif kwamba migogoro katika sehemu za kazi ni jambo la lazima na litaendelea kuwepo mpaka mwisho wa dunia. Kwa sababu hili ni suala la maendeleo katika mchakato. Kwa hivyo, migogoro ni jambo la lazima.

Ile migogoro ambayo imeshindikana kusuluhishwa kama nilivyosema bado inaendelea kufuatiliwa na kufanyiwa kazi. Pia, sheria imeeleza wazi kwamba waajiri ni lazima wawe na mikataba kwa wafanyakazi wao wale wanaowaajiri. Lakini kama nilivyosema migogoro ni lazima itakuwepo. Kwa hivyo, ukiukwaji mara nyengine unakuwepo ndio maana tukaweka sheria hii kuwalinda, yanaletwa malalamiko na wale wanaobainika wizara yetu inafuatilia na ile ambayo inashindikana inapelekwa mahakamani kwa kupata ufumbuzi wa haki Ahsante.

**Mhe. Aziza Nabahan Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza ambalo nataka kupata ufafanuzi. Mhe. Waziri ametuambia hapa sekta binafsi zipo ambazo hazitimizi masharti.

Kwa hivyo, hao wanaokuwa hawatimizi masharti wanachukuliwa hatua gani. Kama wanachukuliwa hatua je, wanafuata masharti au vipi.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti sekta binafsi kama nilivyoeleza inaongoza katika migogoro na wizara yetu kipitia Kitengo chetu cha Ukaguzi Kazi, tunaendelea kuwachukulia hatua. Lakini ile ya wafanyakazi wenyewe ambayo imeshapita kwenye Kamisheni yetu ya Kazi kama nilivyoeleza, inabidi ipelekwe kwenye vyombo vya kisheria kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za ziada, ili wananchi hao wapate haki zao.

Vile vile, ni ile tu migogoro ambayo inayoripotiwa kwenye kamisheni yetu ndio ambayo inayoshughulikiwa na ile mingine ambayo haishughulikiwi na sisi tutakuwa hatuna uwezo wa kujua nini kinatokea huko.

Kwa hivyo, tunatoa wito kwa wale wasioridhika na jinsi ya utendaji au wanavyofanyiwa na waajiri wao kwa kupitia vyama vyao vya wafanyakazi, wapeleke malalamiko yao ama walete kwenye wizara yetu tutayashughulikia kwa kadri ya uwezo wetu pamoja na mamlaka yetu yanavyotuelekeza.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama.

(a) Kutokana na jibu mama la Mhe. Waziri ametuleza kwamba migogoro yote hiyo zaidi ameielekeza kwenye sekta binafsi. Je, hakuna wizara yoyote ya serikali inayohusika na kama ipo ni ipi.

(b) Kwa mujibu wa takwimu alizotupa kuna migogoro 78 ambayo haijashughulikiwa. Je, imefikia hatua gani au ni migogoro sugu.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, sekta binafsi ndio inayoongoza kwa migogoro na wizara yangu ndio wizara husika inayoshughulikia. Kwa sababu kama tunavyofahamu katika muongozo wa Shirika la Kazi Duniani kuna huu utatu ambao unawajumuisha serikali, waajiri pamoja na waajiriwa. Kwa hivyo, masuala ya kazi wizara yangu ndio yenye dhamana ya kushughulikia yakiwemo na haya matatizo na mengineyo.

Kuhusu migogoro ambayo bado haijashughulikiwa taratibu za kuzishughulikia zinaendelea. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Mjumbe awe na subira na kama anataka kuuliza zaidi nafasi ipo aulize swali mama na wala asingoje nyongeza kwa sababu tunataka kuyafanyia kazi.

**Nam. 90**

**Shughuli Maalum za Baraza la Wawakilishi**
**Kukaguliwa kwa Gwaride.**

**Mhe. Amina Iddi Mbarouk (Kny: Mhe. Salmin Awadh Salmin) –** Aliuliza:

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu. Mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya utoaji wa haki. Kwa kuwa viongozi wakuu wa mamlaka ya utendaji na ile ya kutekeleza utoaji wa haki hukagua gwaride rasmi lililoandaliwa kwa ajili yao na vikosi vya ulinzi na usalama wakati wa shughuli zao maalum.

Je, Mhe. Waziri, kwa nini mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma Kiongozi wake hakagui gwaride rasmi lililoandaliwa kwa ajili yake wakati wa ufunguzi wa vikao vya Bajeti.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa hurusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 kama ifuatavyo:-

Katika nchi yetu hakuna sheria inayoelekeza kuwa lazima viongozi Wakuu wa Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji wa haki wakague Gwaride Rasmi lililoandaliwa kwa ajili yao na Vikosi vya Ulinzi na Usalama wakati wa shughuli zao maalum.

Utaratibu wa kuandaliwa Viongozi Wakuu hawa Gwaride Rasmi wakati wa shughuli zao maalum unatokana na mila na desturi zilizojengeka kwa karne nyingi zilizopita kwa tawala mbali mbali duniani.

Kiongozi wa Mamlaka ya Kutunga Sheria anaweza kuandaliwa utaratibu wa kukagua Gwaride Rasmi wakati wa ufunguzi wa vikao vya bajeti ingawa mila na desturi hazijajengeka hivyo katika sehemu nyingine duniani.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, katika mabunge yote ya *Commanwealth* hakuna ambalo linafanya suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu utaratibu huu haujajengeka katika mabunge mengine duniani.

**Nam. 53**

**Juhudi za Kutafuta Dawa ya Kutibu UKIMWI**

**Mhe. Anaclet Thobias Makungila –** Aliuliza:-

Tokea kugundulika kwa ugonjwa wa UKIMWI wataalamu wa afya wamekuwa katika juhudi kubwa ya kutafuta dawa ya kuutokomeza ugonjwa huu.

(a) Je juhudi za wataalamu zinaonyesha mafanikio gani katika kuipata dawa halisi ya kutibu ugonjwa huu.

(b) Kuna baadhi ya wataalamu wa dawa za jadi au dawa za asili wanadai kugundua dawa ya kuutibu UKIMWI. Je, wataalamu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wanashirikiana vipi na watu hawa kuthibitisha madai yao. Kutokana na hali hiyo wizara inatoa tamko gani kuhusiana na madai hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii –** Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa tokea kugundulika kwa Ugonjwa wa UKIMWI wataalamu wa afya wamekuwa katika juhudi kubwa ya kutafuta dawa kuutokomeza ugonjwa huo.

(a) Juhudi za kutafuta dawa ya Kinga au Tiba ya kutibu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI duniani kote pamoja na Zanzibar bado zinaendelea, lakini hazijaleta

mafanikio ya kutosheleza. Dawa zilizokuwepo mpaka sasa ni (ARV). Hizi zinapunguza makali ya maradhi haya, lakini sio tiba kamili.

Dawa kubwa kwa hivi sasa ni kinga, kuwa waaminifu katika ndoa zetu pamoja na kuepukana na zinaa.

(b) Ni kweli wapo watu wanaodai kuwa wamegunduwa dawa za UKIMWI, Wizara yangu imeshirikiana na wataalamu hao tokea miaka 1987, kwa kila kikundi au mtu aliyejitokeza na madai hayo. Hata hivyo, baada ya kufuatilia dawa hizo zimeonekana kuwa hazina uwezo wowote wa kutibu maradhi hayo na wala hazina uwezo wa kuua Virusi vya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inatoa tamko kuwa hadi hivi sasa dawa ya kutibu UKIMWI haijagundulika, dawa iliopo ni ile ya kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI nayo ni (ARV).

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amelieleza Baraza lako kwamba bado dawa hizi hazijagunduliwa pamoja na kujitokeza watu kusema kuwa wamegundua, lakini ikitafitiwa inaonekana si kweli.

Kutokana na utaratibu wa hawa waganga wa kienyeji hutangaza mpaka kwenye vyombo vya habari kama vile redio na magazeti kwamba tayari wamegundua dawa hizo na kuwatia watu matumaini.

(a) Je, kwa nini serikali haiwakatazi waganga wa kienyeji kutangaza mambo kama haya ambayo si ya kweli.
(b) Kama inashindwa kuwakataza au kukanusha pale wanapotoa yale matangazo yao, kwa nini wizara haitoi mara kwa mara tahadhari hizi kwamba jamani hakuna dawa zilizogunduliwa mpaka Mhe. Waziri anapoulizwa swali ndio anajibu.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna watu ambao wanajigamba kwamba wao wamegundua dawa hizi, kwa nini hatukatazi.

Ni kweli ni sahihi kuna watu wanajiita maprofesa na wengine wanatangazia wazi wazi, pia kuna wanaotia picha zao kwenye magazeti kwamba wao wanao uwezo wa kutibu maradhi mbali mbali. Lakini ukweli ni kwamba hawana uwezo huo wa kutibu maradhi haya ya UKIMWI.

Kwa hivyo, sisi serikali tutachukua hatua zote kwa sababu Baraza hili tukufu limepitisha Sheria maalum ya Tiba Asilia na Tiba Mbadala na ndani ya sheria ile iko wazi kutojitangaza mtu au kutamba na mambo hayo *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba hatua zote tutazichukua katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kuwahakikishia wananchi wetu kwamba bado hakuna dawa ya UKIMWI hadi hivi sasa.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa amekiri kuwepo kwa watu wenye kujigamba kwa kiasi hicho na sheria ipo. Je, wizara yake imechukua hatua gani ya kuwaita watu hao au kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria kwa vile wanaupotosha umma.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba sheria yetu tumeipitisha hivi karibuni na tutaanza kuifanyia kazi mara moja.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, swali langu ni kwamba mwishoni mwa mwaka 2007 tulipata ugeni wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki na tulipata semina ambayo ilielezea masuala ya UKIMWI na walituambia kuna utafiti unaohusiana na chanjo na UKIMWI. Je Mhe. Waziri anaweza kutueleza taarifa hii imefikia wapi.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kuhusu chanjo ya UKIMWI bado haijapatikana, Tanzania Bara tunajua wanafanya utafiti huo na sehemu mbali mbali duniani. Lakini hadi hivi sasa hakuna chanjo wala tiba ya UKIMWI. Ninapenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba jibu hili ndio sahihi, kwa hivyo wananchi wasiweke tamaa kwamba hivi sasa kuna kitu hicho.

**Nam. 26**

**Daladala za Unguja na Pemba Kubeba Idadi Sawa ya Abiria**

**Mhe. Ali Suleiman Ali –** Aliuliza:-

Gari za Daladala aina ya Dungu, zinabeba abiria 15 Unguja, wakati huo huo kwa upande wa Pemba zinabeba abiria 18.

Kwa kuwa Daladala za Pemba zinaweza kubeba abiria 18 bila ya usumbufu wowote na kwa kuzingatia kuwa wizara inayohusika na suala hili ni moja. Je, Mhe.Waziri huoni kuwa ni vyema Daladala zote za Unguja na Pemba zikawekewa idadi hiyo ya kubeba abiria 18.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza. Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 26 kama ifuatayo:-

Ni kweli kuwa huko nyuma kulikuwa na daladala aina ya Dungu za Pemba zilikuwa zinabeba abiria 18 tofauti na Daladala za Unguja ambazo zinabebea abiria 15. Hata hivyo, utaratibu huo kwa sasa umeshafanyiwa marekebisho na ilikuwa unafanyika kwa makosa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ombi lake alilolitoa kwa kuongezwa kwa abiria watu na kufikia 18 kwa gari hizo, wizara yangu inalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi na kama kutakuwa na uwezekano huo, basi tutaangalia suala zima la kuongezeka kwa bei ya mafuta pamoja na gharama za uendeshaji wa gari kwa faida ya wananchi tutafanya hivyo.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote baada ya kuona kwamba ipo haja hivi sasa tubadilike, kwa kuongeza idadi ya abiria kutoka 15 na kufikia 18 hasa tukizingatia yale mazuri yote wanayofanya wenzetu kutoka sehemu za nchi yetu yanayofaa basi tuyaige.

Vile vile ninawapongeza wataalamu wa Pemba katika wizara hii waliokaa na kufikia hukusu kuongezwa kwa abiria kwenye gari za daladala.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hilo zuri ninamwomba Mhe. Waziri atakapokuwa tayari awachukue wale washauri kutoka kule Pemba ambao wameanzisha mpango huu mzuri bila ya bughudha yoyote, kwa ajili ya kumsaidia haraka katika kutekeleza azma hii nzuri ambapo wenye daladala watafurahi na hii itawasaidia wananchi wetu na hasa wanafunzi wanaokwenda skuli bila ya matatizo yoyote.

**Nam. 6**
**Uimarishaji wa Karakana ya Matrekta Pemba**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Ali Abdalla Ali)-** Aliuliza:-

Miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa chini ya Karakana ya Matrekta ya Wawi, Pemba ni pamoja na kutoa ushauri, kuchonga vipuri, kufanya *service* na kutengeneza magari. Hata hivyo, hali ya karakana hiyo hivi sasa ni mbaya sana na kuifanya ishindwe kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, ukosefu huo unachangiwa na wizara kutotoa kipaumbele kwa kitengo hiki pamoja na kukabiliwa na tatizo la kutolipwa pesa zake inazozidai toka taasisi za serikali zenye thamani ya shilingi 160 milioni.

(a) Kwa kuwa deni linalodaiwa kwa taasisi za serikali ni kubwa sana. Je, wizara yako itahakikisha vipi kulipwa kwa madeni hayo.

(b) Kwa kuwa serikali haiingizii fedha karakana hiyo. Je huoni kwamba huku ni kuiua.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kufuatilia ulipaji wa madeni ya taasisi za serikali kwa karakana Pemba, wizara yangu imekuwa ikifuatilia na kuwaandikia taasisi husika, ili fedha hizo ziweze kulipwa.

(b) Ni kweli kwamba serikali haiingizi fedha karakana hiyo kwa sababu imo katika mfumo wa kujiendesha kibiashara kwa maana hiyo, haina kasma katika bajeti ya serikali. Lakini serikali kwa kupitia wizara yangu, bado inaisaidia kwa kuwalipa mishahara wafanyakazi wote wa karakana hiyo.

    Vile vile kuanzia mwaka huu kwa kuwa wizara nayo ililiona hali hiyo, tutaweka nguvu zetu kubwa katika kuisaidia kwa hali na mali katika kurudisha hadhi yake na kuinusuru karakana hiyo isife.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa karakana hii pamoja na ile ya Mbweni zinashindikana kuwekwa pahala pale na serikali na hivi sasa ni miaka mingi sasa, si mashirika wala si idara.

Je, wizara yake ina mpango gani wa dharura kwa ajili ya karakana hizi kwani zinawasaidia wakulima na hali ya chakula ilionekana katika kipindi kifupi kilichopita. Kwa hivyo, wizara ina mpango gani wa dharura ama iwe idara au shirika kikamilifu karakana hizi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu mama ni kwamba hali ya karakana zetu si nzuri ingawa nilijibu kwa ile ya Pemba, lakini na hii ya Unguja nayo pia tumeiona. Kwa hivyo, serikali itafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa litakuwa shirika ambalo litaweza kujitegemea *(Makofi)*.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Mwenyekiti ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa serikali jitihada yake yote inatilia mkazo kilimo hasa baada ya kuwa mataifa makubwa yanayozalisha chakula yalitishia kwamba huenda vyakula vya nafaka vikageuzwa nishati ya mafuta. Baada ya hapo serikali ilijitahidi sana kuimarisha kilimo hasa kwa kuagizia matrekta 10 makubwa na 12 madogo.

Lakini hali hiyo ya uagizwaji wa matrekta wakati karakana ya kutengenezea matrekta kikadharaulika, nini faida ya wakulima na wawe na matumaini gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumhakikishia kwamba serikali haijadharau karakana. Isipokuwa nilichokisema ni kuwa lengo lake kuifanya iwe shirika, ili liweze kujitegemea na katika kumhakikishia suala hilo ndio maana serikali inatoa fedha maalum kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi waliopo pale.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Mwenyekiti ahsante kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa karakana hii ni muhimu na sio tu kwa matrekta lakini pia kwa vyombo vyengine vya usafiri. Kutokana na kipindi kirefu serikali imekuwa ikifanya juhudi, lakini inaonekana imeshindwa na juhudi zake pamoja na kuahidiwa hivi sasa litabadilishwa liwe shirika. Lakini serikali haionekani kuwa na mpango angalau wa kucheza upatu wa kuweza kulipa deni katika hili shirika badala ya kulisaidia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri swali lake Mhe. Mjumbe linachangia kwa sababu serikali haiwezi kucheza upatu kwa ajili ya kulisaidia shirika hili, isipokuwa ninadhani anakusudia yale madeni.

Napenda kumhakishia kuwa pale mwanzoni kulikuwa na madeni ambapo shirika letu lile la Pemba lilikuwa likidaiwa kiasi cha shilingi milioni 160 na mpaka hivi sasa sisi kama Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira tulikuwa tukidaiwa, lakini jumla ya shilingi milioni 58 tayari zimeshalipwa shirika lile.

Sambamba na hilo tunafanya kila jitihada ya kuhakikisha wale washirika wengine wanaodaiwa walipe zikiwemo Vyuo vya Mafunzo, Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi pamoja na Wizara yangu.

**Nam. 14**

**Usomeshaji wa Vijana wa Kizanzibari katika Sekta ya Mafuta**

**Mhe. Ali Denge Makame –** Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kuna matumaini makubwa ya kuwepo mafuta katika visiwa vya Zanzibar na kwa kuzingatia kwamba nchi nyingi zenye rasilimali hiyo ya mafuta zilijiandaa kwa muda mrefu kabla ya uchimbaji, kwa kusomesha wataalamu wake wenyewe kwenye maeneo tofauti kama vile uhandisi, uchimbaji, usimamizi pamoja na uuzaji wa bidhaa hiyo.

(a) Je, Wizara ina mikakati gani ya kuanza kusomesha vijana wa Kizanzibari kwa wingi, ili rasilimali hiyo itakapoanza kuchimbwa, vijana wetu ndio wafaidike na ajira na kipato kitokanacho na raslimali hiyo.

(b) Wizara inajipanga vipi kuhakikisha kwamba azma ya serikali ya kuajiri Wazanzibari katika kila sekta inatimia, pia katika maeneo yote ya sekta ya mafuta, isipokuwa kwenye maeneo ambayo Wazanzibari hawana utaalamu nayo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatayo:-

Kama nilivyosema katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/2009 kuwa wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la *Oil for Development (OFD)* lina mpango wa kuwapatia mafunzo vijana wetu katika fani ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta pamoja na gesi asilia.

Mshauri kutoka Kampuni ya *BRIDGE* tayari ameshatoa ripoti yake na sasa ipo katika Ubalozi wa Norway, kwa maana ripoti ya awali iliyohusu nini hasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahitaji kufanya kwa ajili ya kujiandaa na utaratibu mzima huu

wa utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia. Pia tunatarajia kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Mshauri yatawasilishwa hivi karibuni wizarani kwa ajili ya kuendelea na mazungumzo na shirika hilo pamoja na Serikali ya *Norway*.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawahamasisha vijana waliofanya vizuri katika mitihani ya Kidato cha Sita kwenda kusomea fani hiyo katika ngazi ya Shahada na Stashahada.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili ambalo ni la Wazanzibari, kama zipo ajira ambazo zitakuja kutokeza tutakapokuwa tayari na zitawea kufanywa na Wazanzibari, basi serikali itawaajiri Wazanzibari pekee.

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu serikali imeshapanga mikakati ya kuwasomesha vijana wa Kizanzibari kwa wingi, ili rasilimali hiyo itakapoanza wafaidike zaidi Wazanzibari. Lakini ninapenda Mhe. Waziri atueleze nini hatima iliyopangwa na wizara yake juu ya kulifanya suala hili, hasa sisi tulikuja na Mshauri Mwelekezi. Kwa hivyo tunataka kujua hatima yake ya uchimbaji wa mafuta kwa Wazanzibari.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa swali lake hili kwa maana lina uzito na umuhimu mkubwa sana kwa sisi Wazanzibari.

Kweli kama alivyoeleza yeye mwenyewe kwamba tarehe 18 Septemba 2008, katika utaratibu wa kulifikisha kwenye hatima suala hili, Mshauri Mwelekezi aliletwa mbele yenu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar, ili kupata maoni ya wajumbe wa Baraza hili katika utaratibu wa kumalizia ripoti yake na kuileta serikalini kwa ajili ya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya mwisho ya suala hili aliloagizwa Mshauri Mwelekezi tayari imeshawasilishwa wizarani kwangu. Hivyo, napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili tukufu la Wazanzibari kwamba ndani ya siku chache zijazo wizara yangu itakamilisha Waraka wa Baraza la Mapinduzi, ili Baraza hilo lifanye maamuzi juu ya suala hili.

Yaliyosibu katika kikao chake cha mwisho kabisa Baraza la Mapinduzi limeamua kwamba litafanya maamuzi hayo, lakini kutokana na uzito wa suala hili litaletwa tena mbele ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar kwa maamuzi. Kwa hivyo, serikali itafanya maamuzi na itakuwa juu yenu Wajumbe kukubali au kukataa *(Makofi)*.

Kwa nini serikali ikafanya hivyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nieleze katika Bara la Afrika kuna nchi nyingi ambazo tayari zinavuna mafuta na gesi, kaskazini mwa Afrika kuna Algeria na Libya, Kusini mwa Jangwa la Sahara kuna Chad, Nigeria, Sudan, Gabon, Equatorial Guinea, Angola, Congo Brazzaville, Congo DRC na Afrika ya Kusini. Nchi zilizogundua lakini bado hazijachimba ni Uganda, Ghana, S. Tome and Principe, Mauritania, Western Sahara, Gambia na Madagascar.

Lakini kusini mwa Janga la Sahara nchi zote zilizogundua mafuta haziko salama, kwa maana watu wao wanauwana kila siku kutokana na neema hiyo waliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Nchi nyengine zinasumbuliwa na mikataba mibovu. Sasa kwa misingi hiyo, Baraza la Mapinduzi likaona hapana, hili jambo linawahusu Wazanzibari wote. Ni vyema wakashirikishwa Wazanzibari wote katika maamuzi yake.

Sasa, niwashauri wajumbe wa Baraza hili tukufu, kwa vile suala hili litakuja tena hapa, ni vyema tukajiandaa kwa maana sisi ndio tunaowawakilisha wananchi wa nchi hii, na watakuwa na matumaini makubwa sana kutusikiliza wakati tunalijadili, na tunategemea katika kikao chetu cha mwezi wa April, serikali italeta taarifa hii hapa. Kwa mnasaba huo, ni vyema tukajiandaa. Serikali itajitahidi kuweka wazi kabisa na kuleta taarifa zote tulizokuwa nazo mikononi kama tulivyofanya kwenye semina yetu. Kuna makabrasha mengi, kuna *Draft Reception Report,* kuna utafiti uliyofanywa na mshauri mwelekezi kwenye PSA *(Production S**earing A**greement),* yale makubaliano baina ya kampuni na nchi kwa serikali. Kuna *draft final report* yenyewe, kuna ripoti inayohusiana na masuali ya mazingira, sasa hizo zote zitaletwa mbele yenu mpate muda wa kuzipitia na hatimae mzijadili na kufanya maamuzi.

Jengine ambalo litatusaidia, ni vyema wajumbe wa Baraza hili tukufu wakapitia Katiba ya Zanzibar kwa kina Katiba. Katiba yetu imeandikwa vizuri, ni vyema tukaelewa mamlaka ya nchi yetu ndani ya Katiba yetu na maelekezo, hasa katika masuala ya uchumi. Nini Katiba inaelekeza kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye masuala ya uchumi na ya kijamii na mengineyo. Ni muhimu pia tukapitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni muhimu kupitia sheria yetu ya masuala ya ardhi, Sheria namba 12 ya mwaka 1992. Zote hizo ni muhimu katika maamuzi yenu waheshimiwa wajumbe ikiwemo Sheria ya Mazingira, Sheria ya kodi ya mapato na makampuni.

Lakini pia ninawashauri kuwa kuna kitabu hichi kilichoandikwa na Rais wetu Mstaafu Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi kinaitwa *The Publish* miaka 30 ya dhoruba kipitieni kitaweza kutusaidia.

Vile vile nawashauri kuna *paper* nyingi zimeandikwa na viongozi mashughuri inayohusiana na masuala haya ya Muungano, kuna kamati ya Mhe. Shamhuna, Kamati ya Mhe. Amina, Kamati ya Mhe. Ramia n.k.

Pia, ninawashauri kuna *paper* moja ambayo nimeiona mimi imeandikwa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary ambayo inaitwa mgogoro wa kikatiba Tanzania ni kutokana na waandishi wetu wa Katiba au watekelezaji wa Katiba hizo. Hiyo ni *paper* ambayo ameitoa Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Nyengine ambayo nimeihisi imeandikwa kwa kina na inaweza kuwa na manufaa hii inaitwa Hatma ya Zanzibar na Mustakbar wa Muungano imeandikwa na Mhe. Waziri Kiongozi Mstaafu, Seif Shariff Hamad inafaa tuipitie.

Vile vile kuna kitabu chengine kinaitwa *Pan African Museum of Fragmentism.* Hiki ni kitabu kilichoandikwa na *Professor Issa Shivji. M*imi nina mashaka nacho kidogo tu, lakini si kila kitu unachokisoma ni lazima ukipende, ikiwa kinasaidia ni vyema tukakipitia kwa maana amezungumzia Mapinduzi Matukufu ya Januari 12 kama ni uvamizi tu, na amejilazimisha kukataa kwamba Afro Shirazi Party kilikuwa chama cha siasa kilichokubalika na mapinduzi yale yalikuwa ya watu. Lakini si vibaya kitabu chake nacho pengine kikaweza kusaidia wajumbe wa Baraza hili tukufu katika maamuzi ambayo pengine tutakabiliana nayo katika mwezi Aprili mwaka huu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi nakuomba hizo nyaraka ambazo ziko mkononi mwako tukaweza kuzipata na zile za Mhe. Abubakar na Maalim Seif, kama zipo ni vizuri tukasaidiana na kugawa kwa wenzetu vipi utafanya, mtashirikiana. Lakini naomba zipatikane.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza nimsifu sana Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na hasa pale bajeti ya mwaka jana Wazanzibari waliposhikana, kwa sababu sijapata kuona hata siku moja pande zote mbili kumuunga mkono katika kupitisha bajeti isipokuwa bajeti hii. Walipitisha kwa moyo mmoja baada ya kuona Mhe. Waziri alitamka maneno ya ushujaa.

Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 wa Katiba hasa kifungu 23(3), nitapendelea kusoma hapa naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

Kifungu 23 kinasema.

"Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya taifa lao".

Lakini pamoja na haya tuna Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hata hivyo kuna kifungu cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachosema gesi na mafuta ni mambo ya Muungano, hivyo wabunge wetu watakuwa tayari kutetea Katiba hii au watatetea kifungu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kueleza nilipokuwa nikijibu swali la Mhe. Najma Khalfan hili jambo ni uzito ni jambo zito, linalolenga kwenye mustakbali wa sisi Wazanzibari tulio hai leo, na vizazi vyetu vinataka umakini na mshikamano wa hali ya juu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nalishukuru sana Baraza letu tukufu la Mapinduzi kwa kufanya maamuzi ya hekima, kwamba hili suali litahitaji Wazanzibari wote kushiriki na kuliamulia, halina siasa lina Wazanzibari.

Namshukuru Mhe. Ame Mati Wadi kama kawaida yake ameona maelekezo ya Katiba, niongezee zaidi kusema kwamba Katiba hiyo hiyo, inaielekeza serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar kudhibiti uchumi, sisi Wazanzibari muongozo wetu ni Katiba yetu ya Zanzibar, Katiba hiyo hiyo pia inaielekeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kudhibiti sehemu zote nyeti za uchumi.

Katiba hiyo hiyo, inaelekeza kwamba hakuna sheria yoyote itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isipokuwa mambo yaliyokuwa ya Muungano na hata ikitunga sheria hiyo inapaswa kuletwa hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi na Waziri husika ili kuthibitishwa, pia zinapotungwa kanuni pia Zanzibar kushiriki kikamilifu na inahitajika *two-third majority* katika maamuzi yake.

Sasa masuala ya gesi asilia na mafuta hayakupata kuwa ndani ya makubaliano ya awali ya Muungano baina ya watu wa Jamhuri ya Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika. Hayo yote nitakuja kuyachambua na kuyajadili na kuyafanyia maamuzi kwa niaba ya Wazanzibari wote. Nimewaomba msome kwa sababu la msingi ni hoja, sio jazba. Naamini hoja zipo, uwezo wa kujenga hoja wawakilishi tunao kwa sababu wananchi wetu watataka watusikilize, na wote watasikiliza pamoja na dunia itatusikiliza. Sasa tunao watu wameshiriki kutunga Katiba hizo.

Sasa naomba kila mmoja wetu ajiandae Mungu akipenda tutakuja kulizungumza mwezi wa Aprili mwaka huu. Ahsante sana.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kabla Mhe. Ame Mati Wadi hajauliza swali lake kulikuwa kuna ufafanuzi kidogo kuhusu makabrasha na makaratasi mbali mbali alikuwa anataka kutueleza Mhe. Waziri, kwa hivyo nilikuwa nakuomba Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako umpe nafasi atuambie.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, kumradhi nimesahau kulisema hili, hizi taarifa na *paper* nilizokwambieni zipo kwa maana ya Mhe. Abubakari Khamis, huyu hapa anaweza kutusaidia kupata *paper* yake. Nyinyi kwa upande wa Chama cha upinzani huko, nafikiri *paper* aliyoandika Waziri Kiongozi Mstaafu, Mhe. Seif Shariff Hamad mnaweza kutusaidia. Hivi sasa nyaraka nilizokuwa nazo mimi mkononi ni mali za Baraza la Mapinduzi pamoja na ripoti zote zile za mshauri mwelekezi, siwezi kuzitoa mpaka nipate idhini ya Baraza la Mapinduzi.

Lakini nimesema kwamba serikali haina cha kuficha, kwa hivyo tutakapomaliza kikao cha Baraza la Mapinduzi nitaomba Baraza lile tukufu liniruhusu kupata nyaraka zote ambazo zitawasaidia wawakilishi katika maamuzi zije kwenu mapema ili mpate kuzipitia, kwa sababu bila ya kuja zile nyaraka mtashindwa kufanya maamuzi.

**Nam. 104**

**Rais Kuhutubia Wananchi Kupitia Vyombo vya Habari.**

**Mhe. Ame Ussi Juma** **-** Aliuliza:-

Itakumbukwa kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, anawahutubia wananchi wa Tanzania kuhusu mambo mbali mbali ya maendeleo ya nchi kila mwisho wa mwezi kupitia Televisheni, na magazeti pia huandika hutuba zake baada ya kuzitoa katika Televisheni.

(a) Kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Je, huoni kwamba ipo haja kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuata tabia hii.

(b) Kama ipo, Je, kuna hatua zipi zilizochukuliwa ili wananchi wakaweza kufahamu maendeleo ya nchi yao kupitia mfumo huu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi –** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti nakubaliana kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete huwa anawahutubia wananchi wa Tanzania kuhusu mambo mbali mbali ya maendeleo ya nchi kila mwisho wa mwezi kupitia Televisheni na magazeti na vyombo vyengine.

Naomba niseme kwamba kila kiongozi ana staili yake ya utawala na pia ana staili zake za kuendesha nchi mbali ya zile *principle* zilizokuwepo, lakini kwa kuzingatia misingi ya utawala Bora kama alivyosema Mhe. Ame Ussi, ni busara kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuzungumza na wananchi kuhusu mambo mbali mbali ya maendeleo ya nchi, na yeye huwa anafanya hivyo kupitia kwenye Televisheni na redio na pia huandikwa kwenye magazeti, lakini si kila mwisho wa mwezi kama utaratibu anaofanya Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete.

Lakini pia naomba nitoe mfano mwengine, huko huko Tanzania Bara Marehemu baba wa taifa na yeye alikuwa na utaratibu wake. Yeye alikuwa anawahutubia viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kila mara kukiwa na habari nzito au mambo ya maendeleo, basi hualika mikutano viongozi wa Mikoa wa Dar es Salaam kwa maendeleo na matatizo.

Sasa tukirudi kwenye suala la msingi niseme kwamba utaratibu anaofuata sasa hivi kwa Rais wa Zanzibar kwa kuwasiliana na wananchi juu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na maendeleo na kiuchumi, ni wa kuzungumza na wananchi kila anapofanya ziara katika maeneo yao kama katika ufunguzi wa miradi ya maji, skuli, vituo vya afya n.k.

Mbali ya mialiko ambayo Mhe. Rais huwa anaalikwa mara kwa mara huwa anahutubia na kuelezea hatua za maendeleo zilizofikiwa, niseme kwamba Mhe.Rais mara nyingi pia huwa anapoalikwa hubadilishana mawazo na wananchi na hutoa kauli au taarifa za maendeleo ya nchi pale yalipofikia. Kwa hivyo niseme kwa kumalizia kwamba baadhi ya taarifa za hotuba hizo au zote mara nyingi zinaandikwa kwenye magazeti kama hukupata kusikia kwenye vyombo *live*, basi unaweza kusoma kwenye gazeti. Ahsante.

## SHUGHULI ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Maonyesho

**(***Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kwa asubuhi hii ya leo mimi nikaweza kuchangia huu mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Bodi ya Senda na Filamu za Maonyesho.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kuleta mswada huu muhimu zaidi kwa kulinda mila silka na utamaduni wetu, uundwaji wa bodi hii kama alivyoeleza Mhe. Waziri kwamba Mswada huu haufuti ile sheria iliyokuwepo isipokuwa amejaribu kuona yale mapungufu yaliyokuwemo kwenye ile sheria, ndio maana akaleta mswada wa kuanzisha bodi ambayo itaweza kuhakiki filamu pamoja na maigizo mbali mbali.

Kwa hivyo nimpongeze kwa kuliona hilo kwa sababu sheria tunakuwa tunazitunga, lakini baadae katika utekelezaji ndio tunapoanza kuona yale mapungufu, kwa hivyo baada ya kuona yale mapungufu Mhe. Waziri ameleta mswada huu na tunashukuru waheshimiwa wengi wamechangia vizuri kabisa katika kuhakikisha kwamba tunaiboresha hii sheria, lakini vile vile michango yao inaonyesha kwamba wanakubaliana na Mhe. Waziri kwa hii hoja ambayo wamekuja nayo.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nizungumze kidogo tu kwa sababu jana Mhe. Waziri alipokuwa na dharura kidogo aliniachia nikaimu kidogo, sasa kulikuwa na michango ambayo ilikuwa ikitolewa nilikuwa najaribu kuinukuu na mingi yao ilikuwa ni mizuri. Tangu nilipokaa hapa sijaona mchango wowote ambao labda hauna nia njema ya kuweza kuboresha huu mswada, michango yote ilikuwa mizuri, lakini kuna baadhi ya mambo madogo madogo nitaomba niyatolee ufafanuzi, ili kuweza kumsaidia na Mhe. Waziri atakapokuja ku-*wind up.*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk swahibu wangu alizungumza sana suala la utamaduni na silka inavyomong'onyoka humo mitaani na kidogo alitoka nje ya mswada, kwa sababu kama tulivyosema ile sheria bado ipo na haijafutwa, lakini hapa kumeundwa chombo tu na hichi chombo sio kwamba kitabeba yote isipokuwa yale maeneo ambayo ile bodi kama ilivyoainisha katika zile kazi zake.

Kwa hivyo, alijaribu kuzungumzia kero zilizojitokeza hasa nyakati za sala, alitoa mfano kwamba kuna mabaa haya ya mitaani ambayo wakati mwengine watu wanajiandaa kwenda kwenye swala wao tayari na magoma yao wanapiga. Sasa kimsingi hili serikali yetu halitoiachia bodi peke yake, serikali iko makini kwa suala hili na hivi karibuni tayari kuna baadhi ya wananchi walikuja kulalamika na wameleta malalamiko yao kupitia kwa sheha wao na hayo malalamiko tumeshaanza kuyafanyia kazi. Wananchi wa shehia ya Miembeni walitishia kwamba kama serikali haitochukua hatua za haraka, basi inaweza kuvurugika amani na kwa kuwa tulikuwa na uthibitisho wa sheha, basi serikali tayari tumeshaanza kuchukua hatua.

Serikali haichukui hatua tu kwa sababu wananchi wamenza kulalamika, lakini baada ya wananchi kulalamika huwa tunafanyia kazi na tukiona kwamba kweli hali imekuwa ni mbaya, basi serikali inachukua hatua. Kwa hivyo, kulikuwa na baa mbili ambazo zimelalamikiwa moja ni baa ya Jozani na nyengine inaitwa Jitini zote za Miembeni, tayari serikali imeshamuagiza mwenyekiti wa bodi ya leseni ya vileo kuzifunga mara moja baa hizo. Kwa kuwa eneo lile tumejaribu kufanya utafiti, maadili yanakiukwa kwa sababu zile baa ziko ndani ya mitaa, kimsingi mambo yanayofanyika pale ni hatari tena hatari sana.

Kwa taarifa tulizokuwa nazo na nimejaribu kuzifuatilia tuligundua kwamba kuna watu huwa wao wana kazi ya tenda ya kuja kuwaleta pale, na watu wenyewe sio raia wema. Kama walivyozungumza baadhi ya wajumbe, kwamba Mzee Ali Hassan Mwinyi alipotangaza Zanzibar ni njema atakae aje, basi waliingia wema mpaka na wabaya, sasa sisi tuliowakaribisha wema, wabaya hatuwezi kuwakaribisha.

Mhe. Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Abass Kandoro yeye baada ya kuona hali imekuwa mbaya katika pahala ambapo panaitwa Uwanja wa Fisi, basi alikwenda mara moja na Uwanja wa Fisi akaufunga. Sasa wale waliokimbia Uwanja wa Fisi wengine walipanda boti wakakimbilia Zanzibar na wengine tumegundua kwamba waliokimbia Uwanja wa Fisi baadhi yao wakafikia Miembeni. Kwa hivyo tumemwagiza mwenyekiti wa bodi ya leseni kwamba katika leseni ya mwaka huu 2009, baa zile mbili za Jitini na Jozani zisipatiwe leseni.

Tunaangalia ikimaliza mwezi wa Januari, sasa kuanzia mwezi wa Februari utekelezaji wa agizo la serikali kama limetekelezwa au vipi na kama halikutekelezwa, serikali itatumia namna nyengine yoyote ya kuhakikisha kwamba baa zile zinaondoka kabisa, na hali ya utamaduni inaendelea kurudi kama kawaida yake katika eneo lile. Kwa sababu hata matendo maovu ya madawa ya kulevya, yaani pale pana biashara kubwa kubwa za dawa za kulevya pamoja na bangi, pamoja na kuuza hawa makahaba, kwa kweli hali ilikuwa sio nzuri. Kwa hivyo, hatuachii tu kama mlivyosema kwa sababu mmesema bodi ipewe nyenzo sasa nyenzo sio pesa tu, lakini vile ni kuwa na maamuzi ambayo yataweza kuheshimiwa, sasa na serikali haitoiachia bodi peke yake.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea katika kuchangia Mhe. Said Ali Mbarouk jana alitoa jambo hata na mimi lilinipa wakati mgumu sana na nikajaribu kujiuliza kweli Zanzibar tumeshafikia hatua hii. Sasa kwa kuwa niliachiwa kazi na Mhe. Waziri, sikutaka kazi ile

aje aifanye yeye, nikaona niifanye mimi mwenyewe kwa sababu suala la kuhadithiwa sio suala la kuona wewe mwenyewe.

Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumzia mfano uliotokea pale Wete kwamba bwana harusi sasa sijui niite na bin harusi, kwa sababu wote ni wanaume, walitaka kuoana pale Wete na wananchi baada ya kuona harusi inaandaliwa wakaenda kuwavamia ili ile harusi ivunjike. Lakini mshangao wa Mhe. Said Ali Mbarouk alisema kwamba kitu alichoshangaa yeye kwamba yule bin harusi kuna lugha wanaitwa lakini sitaki kuitaja hapa hadharani, lakini nafikiri nikizungumza mchumba, mchumba kwa wenzetu wale wa Mombasa wanajua nimekusudia nani.

Sasa huyu bin harusi ambaye ni mwanamme alikwenda kushtaki kwamba amedhalilishwa na ameingiliwa katika uhuru wake na ametoroshwa kwa hivyo kesi iko Mahakamani. Sasa mimi nikajiuliza kweli Mahakama yetu inaweza kukaa ikasikliza kesi ya mwanamme aliyetaka kuolewa na mwanamme mwenzake. Badala ya kwamba yule alipokwenda kufungua kesi pale pale walikuwa wamfungulie *charge* na wamweke ndani, lakini baada ya kufuatilia naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Tarehe 15/5/2005 ilifunguliwa kesi Nam. 28 katika Mahakama ya Wete. Katika kesi hiyo washtakiwa alikuwa ni Bw. Ayoub Ismail Moh’d, Bw. Masoud Alawi Ahmed, Bw. Rashid Hemed na Bw. Humoud Thanai. Makosa waliyoshtakiwa ni kumtorosha mvulana kwa mujibu wa kifungu cha 150(b) Sheria Nam. 6 ya mwaka 2004, kesi hiyo ndio iliyofunguliwa.

Kesi ya pili ilikuwa ni shambulio la aibu, kwa hivyo tukio hili kwa mujibu wa maelezo ya yule aliyekwenda kushtaki, alisema kwamba alikuwa na *birthday* yake ambayo aliwaalika marafiki zake mbali mbali, miongoni mwa marafiki hao mmoja ni kutoka Mombasa. Kwa hivyo, alipokuja pale kwenye ile *birthday* kabla haijafanyika, katika shamra shamra akasema kavamiwa na watu asiowajua na wakenda kumpeleka katika eneo. Kule walikomchukua akasema kavuliwa nguo na kuangaliwa sehemu za kukalia kwa sababu walisema kwamba amepaka hina.

Sasa kuna mambo mengine sisi tunaopewa dhamana tunatakiwa vile vile tuwe tunatumia na akili sio tusikilize mtu tu vile anavyosema. Kwamba baada ya kuvuliwa nguo akaangaliwa kwenye makalio amepakwa hina. Sasa ilikuwaje mwanamme mpaka hiyo hina ikapakwa kwenye makalio. Sasa hali kidogo ilikuwa sio nzuri, lakini kwa kuwa yeye mwenyewe kaona ile ni fahari kwake, aliamua kwenda kushtaki. Polisi kawaida mlalamikaji yoyote lazima apewe haki yake. Kwa hivyo kaitwa pale kusikiliza, na kesi ikafunguliwa, baada ya kufunguliwa ikaenda na baadae ikafutwa. Kwa hivyo, ile kesi sasa hivi haipo tena, sasa mimi nilifikiri inaendelea ili na sisi tuwe karibu zaidi kuifuatilia kwa sababu Mahakama ina uhuru wake hatutakiwi tuingilie uhuru wa Mahakama hasa kama haijatoa maamuzi.

Lakini vile vile na sisi ingetupa nafasi kufuatilia hasa huu mwenendo wa hii kesi ungelimalizika vipi, kitu ambacho ninakiomba kwamba inawezekana yule mwanamme aliyesema kwamba anafanya *birthday* yake inawezekana labda ile dhamana ya wananchi

wa pale siku ile ndio alikuwa anakuja kuolewa. Kama kweli alipakwa hina sehemu hizo ambazo alikwenda kumtizama, kwa sababu biharusi tunajua anapakwa hina mikononi, miguuni, hutiwa na wanja. Sasa yeye kwa kuwa mwanamme hapaswi kufanyiwa vitu kama hivyo, kama kweli alipakwa hina, basi kama mimi ndio ningekuwa Jaji basi ningesema kweli wewe ulikuja kuolewa na leo nitakufunga.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ninachokiomba kwamba sisi ndio wawakilishi wa wananchi na tunakaa na raia wetu katika maeneo yetu. Tusijaribu kuchukua sheria mikononi mwetu. Vyombo vya sheria vipo. Wanaume kwa wanaume kuoana kwa hapa Zanzibar hakuna sheria hiyo. Kwa hivyo, nadhani raia wale walikuwa hawapaswi kufanya nguvu. Wangekwenda kuripoti polisi na baadaye wale wangekwenda kuchukuliwa na wale waliopewa mamlaka na sheria kwamba wanao uwezo wa kumkamata mtu.

Sheria tunazitunga hapa kuona nani ana ruhusa ya kumkamata mtu na nani hana ruhusa hiyo. Sasa raia bado hajawa na ruhusa ya kumkamata mtu. Hili limetokezea na wananchi wamekuwa na nia njema ya kulinda mila na silka, ila utaratibu ambao wameutumia ulikuwa sio mzuri. Mara nyengine likitokezea kama hili, basi naomba raia waweze kuchukua taratibu za kisheria ili yasije yakatokezea kama hayo. Haya mambo ya kwenda kufunguliwa kesi kila siku ukaacha shughuli zako nenda rudi hata kama ulikuwa huna kosa, lakini ule usumbufu tu peke yake unakuwa haupendezi.

Mhe. Mwenyekiti, mila na silka bado tunayo tunayo nafasi ya kuweza kuilinda. Ingawa baadhi ya wengine wanasema tumechelewa, lakini bado hatujachelewa kwa sababu sisi ndio tunaoishi na sisi ndio tunakaa na watoto wetu mitaani, kwa hivyo bado tunayo nafasi. Kama alivyosema Mhe. Zakiya alitumia msemo wa Baraka Obama kwamba "*yes we can"*. Ni kweli kwamba tutashirikiana kwa pamoja, jamii yetu tukaielimisha na tukawaelekeza wajaribu kufuata sheria za nchi, basi haya yote yatawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wajumbe wa bodi hii, itakuwa na kazi kubwa ya uhakiki wa filamu, kuangalia zile ambazo zimeshaingia nchini. Kama walivyosema baadhi ya wajumbe, sasa hivi kuna kanda nyingi sana. Nyengine zinaweza zikawa hazikuridodiwa Zanzibar, lakini wao wenyewe wale wenye *internet café* au wale wenye studio za kurikodi CD, akishapata mkanda pengine umeingizwa kwa njia sio za kisheria baadaye baadaye akaufanyia *production* pale pale.

Anaweza akawa na CD moja akazitoa zaidi ya 500 au 600 akaweza kuziuza. Kazi hiyo ya udhibiti ni ngumu na tunaomba tuwasaidie. Kwani bodi itakuwa na watu wachache, lakini wataweza kufanya kazi vizuri zaidi watakapoweza kupata taarifa kutoka kwa raia wema ambao wanaona maadili yanakiukwa sehemu fulani kutokana na sanaa fulani inafanywa na inakuwa haiendi sambamba na utamaduni wetu. Tunahitaji tuwape mashirikiano makubwa ili kuweza kuliwezesha hilo.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nasikiliza hizi redio zetu za FM, ambazo ziko nyingi sasa hivi. Wakati wa saa 3:00 au saa 4:00 wanakuwa na vipindi vyao ambavyo unakuwa unapiga simu na unatoa maoni yako. Wanajaribu kutafuta mada na wanakuwa wanaiongelea. Siku moja walikuwa wanaongelea masuala ya wanafunzi wa vyuo vikuu

jinsi ya vurugu, utamaduni na mambo mengine. Wakasema kwamba sasa hivi huko katika vyuo vikuu ndio yanapokiukwa maadili, lakini sio vyuo vikuu vilivyokuwepo Zanzibar, ni vile vya Tanzania Bara. Wanasema inapofika nyakati za usiku kuna mambo ya ajabu huwezi ukategemea kwamba wale ni wasomi wanaofanya mambo kama yale.

Akatoa mfano wakasema, kama kuna akina dada fulani ambao walikuwa wanakoga, wakachukua simu zao wakajirikodi wenyewe. Pengine bila ya makusudio unajua mambo ya simu unaweza kuficha vitu kama tulivyozungumza jana. Sasa hivi mtoto mdogo hata skuli hajenda lakini anaweza kuichezea simu wewe mwenyewe hujui. Basi inaonesha kama mmoja aliamua kumfanyia mwenzake kwa makusudi, baada ya kuifungua alipoangalia katika ile sehemu ya video nafikiri akaona vile vitendo vyao walipokuwa wanakoga. Akaanza kusambaza kwa watu wengine, matokeo yake baadae wakaja wakaonekana watu wanaoneshana, unamuona fulani? Wakati mwengine simu ya mtu kwenda kuifanyia uhakiki sijui sheria inasemaje, kwa sababu labda itakuwa ni kuingilia uhuru wa mtu na hasa kama huna uthibitisho katika siku ile kuna kitu gani.

Mambo kama hayo tumeyasikia katika vyombo vya habari yamekuwa yakijadiliwa sana. Wakawa wanabishana kwamba labda yule alikuwa siye, labda sura ilibadilishwa kwa sababu siku hizi kuna mambo ya *scanning* na mambo mengine. Lakini hata kama alikuwa siye kwa kuwa lijirikodi mwenyewe anakoga ndio alikuwa yeye. Kazi kubwa sana watakuwa nayo bodi hii. Kama tulivyosema inahitaji busara sana na hasa katika maamuzi yake juu ya mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia ni kwamba tusiangalie wenzetu utamaduni wao uko hivi basi na sisi tukataka uwe hivyo. Mfano kama jana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), alisema kwamba Rwanda kule wana utamaduni wao. Tukiangalia tamaduni za hapa hapa Tanzania kwa sisi Wazanzibari ni matusi makubwa bila ya kwenda Rwanda wala kwenda nchi yoyote. Zile mila zao na kwao wao ni kitu cha kawaida tu, na mtu kama hajafanyiwa hiyo mila bado hajaonekana kwamba ameshaingia katika utuuzima na yupo katika jamii fulani na tayari anaheshimika. Lakini mila zile na ukiangalia kwa hapa mila zetu za Kizanzibari ni kashfa na ni matusi makubwa. Kwa hivyo, suala la mila kila nchi ina utamaduni wake na kila nchi ina mila zake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya nchi za wenzetu tamaduni zao kuna Casino na ukimuona mtu kenda kwenye Casino basi na yeye kenda kuyatafuta. Kwa sababu kwenye Casino mambo yake yanayofanyika ni makubwa sana. Ndio maana nikasema kwamba na sisi kama vile nilivyosema mwanzo kuna yale ambayo yamo ndani ya uwezo wetu bado tutajaribu kuyadhibiti ili yasiweze kutuharibia tamaduni katika nchi yetu na hasa haya mabaa ya mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, zamani tunavyojua sisi kulikuwa na sheria kuhusiana na baa, na baa sio kwamba unatoka ndani ya nyumba unaingia baa, unakwenda unaitafuta. Kwa sababu starehe lazima iwe na gharama na starehe kama haina gharama basi hiyo sio starehe. Leo unatoka ndani ya nyumba unaingia baa, hiyo ndio starehe. Starehe kama hiyo utakuwa unawaudhi wenzako, baada starehe inakuwa karaha. Kwa hivyo, yale mambo ambayo tunahisi sio vizuri kuyaona kila mtu, basi ni vyema yakawa yapo maeneo ya mbali kwa

wale ambao wanakwenda kule wao wenyewe wanakuwa wameshajibagua kwamba sisi ni watu wa aina hii. Lakini isiwe tunawachanganyisha na watu wa aina nyengine.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na tunaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi niweze kutoa maoni machache katika mswada huu. Nimesimama hapa kwa kuona huu mswada una umuhimu hasa kwa jamii ni mazungumzo ambayo tunazungumza sana katika hili Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mambo machache. Mswada huu madhumuni makubwa ni kuhakiki filamu au kanda katika kuhifadhi mila, silka, tamaduni na maadili ya Mzanzibari. Mimi nadhani jana Mhe. Haji Faki Shaali alizungumzia kwamba sio kulinda tu bali ni turejeshe haya maadili kwani hivi ni vitu ambavyo vilikuwepo tokea zamani.

Mhe. Mwenyekiti, hizi mila zetu, silka, tamaduni, maadili, mambo haya ni kama sheria. Jambo lolote ambalo lipo katika mila basi lina nguvu. Tukachukulia mfano wazee wetu mila zao ilikuwa kama mtu kawekwa kizuka utakuta mambo anayo wekewa ni mengi sana na inakuwa ni mikakati mikubwa. Sasa kutokana na kwamba watu wamesoma na wamefunuka kuweza kutambua ni mambo gani anayofanyiwa kizuka. Kizuka alikuwa anatakiwa asichungulie hata nje. Lakini utakaposoma kwenye sheria ukishajua kumbe kizuka desturi yake ipo hivi, tayari umeshaelimika. Lakini bado mila zile zipo kwa wazee wetu mpaka kesho na utakaposimama mtoto kama mimi na nikazungumzia kwamba masharti ya kizuka ni haya na haya, mzee tayari anaona umeshakiuka mila zao. Kwa hivyo, mila inakuwa kama sheria.

Mhe. Mwenyekiti, suala la hizi kanda kila mmoja alizungumzia kwamba zipo na zinauzwa kama njugu kwenye nyungo, hivi sasa kwa kweli ni mtihani. Jana tulivyotoka asubuhi kufika Kikwajuni tu nimo ndani ya gari kaniletea kanda anauza ananiambia "mama kanda hizi zinauzwa hutaki wewe?" Kwa hivyo, nathubutu kusema kwamba bodi ina kazi kubwa tena kubwa sana. Mimi nahisi cha msingi labda zipigwe marufuku kwanza kuingizwa na zilizokuwepo bodi iwe na kazi ya kufanya utafiti. Lakini ikiwa kila siku zinaingizwa haya mambo kila siku yatapamba moto.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja nashukuru Mhe. Waziri keshalitolea ufafanuzi na mimi ilikuwa ndio kiu yangu kubwa, habari ya kupigwa ngoma wakati wa ibada. Hii pia tunachukua katika baadhi ya mila zetu hapo nyuma. Zamani nakumbuka muadhini akiadhini basi watu wote wanakaa upande. Ikilia honi watu wanakaa upande hendi mtu. Tunaweza kusema kwamba hili ni jambo la kuelimishwa ingawa tunaliona ni jambo la masihara.

Mimi siku moja nilikaa na babu yangu nikamuuliza hivi, huyu muadhini akiadhini ukenda kuna tatizo gani? Akaniambia "umeuliza swali zuri mjukuu wangu". Akaniambia

"anapoadhini muadhini ikiwa unakwenda kunakuwa na mashetani wanakwenda mbio. Sasa ikiwa wewe unakwenda anaweza shetani yule akakupiga kikumbo". Kwa hivyo, kila mmoja alikuwa ana hofu na hili ukiliangalia linaingia kwenye mantiki.

Ndio maana unapoambiwa pale anapoadhini muadhini ukae upande kwa sababu shetani anaukimbia ule ukelele wa adhana. Hii ilikuwa ni mila yetu tumeiweka lakini hakuna sasa hivi. Mimi nahisi kuna mambo ambayo yanahusu na jamii tukae tuelimishwe na tuwaelimishe wenzetu. Hili mimi nahisi ni rahisi sana kama alivyosema Mhe. Zakiya kurejesha mila zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hili suala la mavazi. Kwanza nawashukuru masheikh wetu wamefanyakazi kubwa. Ingawa bado huwezi kuwapata wote, lakini mihadhara na jitimai watu siku tatu wanakwenda kukaa pale wanaelimishwa jinsi gani unywele wako mmoja ukionekana matatizo yake na athari yake. Wanawake wanalia sana. Wanawake wengi siku hizi unawakuta wamevaa mashungi na mitandio yao. Wengi unaowakuta wapo kichwa wazi ndio wale ambao wenzetu wa upande wa pili. Mtu akitoka huko akirudi hata akiwa kavaa nguo gani lakini ushungi wake kavaa kichwani. Ningeiomba bodi ikashirikiana nao ili maadili yetu tukaweza kuyafufua kwa kiasi fulani, yasipotee yakazidi kuzama, tupo hali mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wageni kama walivyozungumza wenzangu hawa ndio wanaosababisha haya. Mila zetu Wazanzibar, silka zetu, tabia zetu tunazijua wenyewe, watoto wetu tunajua jinsi ya kuwaelimisha na tunaambiwa udongo upate ulimaji. Mtoto unamuelimisha nyumbani vizuri, akitoka nje mitaani huko akiona mambo tayari na sisi wigo tumeshaiga. Bodi itakuwa na kazi kubwa juu ya kutafiti haya mambo ya filamu.

Leo tuchukulie haya mambo ya harusi zetu. Hakuna hata mtu mmoja ambaye anakumbuka hapo zamani kwamba mtoto aende akalale huko halafu akakamatiwe ndio akaolewe. Hizo sio mila zetu Wazanzibari, hata siku moja. Tunasikia wenzetu waliokuwa Bara huko mtu akishakuchezwa unyago tayari anaachiwa huru. Hapa kwetu hayo hayapo. Lakini sasa yameshaingia na tunayo. Hakuna hata Mzanzibari mmoja anayesema kwamba mimi harusi ya kukamatiwa naifurahia, hakuna anayetaka hayo, wimbi hili tunalo sasa hivi. Hii inatokana na kuwa mila na desturi zetu zote zimepotea hazipo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo serikali ina sehemu yake na kuna mambo na sisi wenyewe jamii tuna sehemu yetu. Kwa hivyo, niseme labda kwa kuwa tulikosea sana hapo nyuma ndio maana mitihani hii yote ikawa imetukuta. Lakini *Inshaa Allah* tutakaa pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika sehemu hii ya sanaa jinsi ya kufanya utafiti katika michezo ya kuigiza. Kuna kipindi kimoja katika TVZ kinaitwa mpambano. Kama nilivyosema kwamba udogo upate ulimaji. Watoto wadogo sana kuanzia miaka sita labda mpaka miaka 15. Ni kipindi kizuri, watoto mule wanakwenda kufanyiwa kama chemsha bongo. Lakini inafika wakati wanaambiwa sasa hivi ni wakati wa kuonesha vipaji vyenu watoto. Wanaweza kuambiwa kwa mtaa, mfano mtaa wa Kwahani na Kwaalinatu au mtaa wa

Jang'ombe na Mwanakwerekwe. Wanatoka pale wanakuja watoto wa upande mmoja wanawaonesha vipaji vyao na wanakuja watoto wa upande mwengine wanaonesha vipaji vyao. Kwa hivyo, mimi ningeomba vile vipaji vyao vifanyiwe uhakiki.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita natokea tu hivi tayari upo ule mpambano nikaona watoto wa upande mmoja wameonesha kipaji chao cha kuendesha baiskeli, yuko juu anaruka ruka na kibaskeli cha ringi moja. Upande wa pili wao wakaonesha kipaji chao kama ni mchezo wa kuigiza, lakini ule mchezo unapotosha. Wakati yule mtoto umeshamuonesha vile, anapoondoka pale anaondokea na lile lile sio kama anaondoka pale na lile analiacha pale pale, sio kweli. Anaona hii tayari imeshakuwa dili na anaona ule mchezo ulioneshwa pale ndio unafaa. Kwa kweli haikufurahisha hata kidogo. Kuna mwanangu mmoja akasema hii! Mchezo haufai huu. Ni mtoto mdogo, lakini kasema haufai na ni mchezo unaopotosha, unavunja maadili yetu na unavunja mila na silka zetu. Leo umeoneshwa kwenye TV na ni mtoto wa miaka 6 ndio aliyekwenda kuigiza mchezo ule.

Wameigiza kwamba mwanamke anauza maandazi kajitanda kanga yake nzuri. Mara wakatokea watoto wawili wameshakula unga, mmoja akasema nna njaa bwana. Baada ya kufika pale kununua maandazi hakununua, basi akambaka pale pale. Yule mtoto akitoka pale mtoto wa kiume wa miaka 6 kapata funzo juu ya hilo, hakupata funzo. Kwa hivyo, mimi ningeliomba vitu kama hivi viangaliwe, na hii michezo ya kuigiza iangaliwe vizuri tena kwa kina. Kila mwakilishi aliyesimama hapa anasema kwamba bodi inakazi kubwa, ni kweli.

Pili nakuja katika sehemu ya ngoma kulinda maadili. Ingawa sasa hivi imepungua kidogo mambo ya harusi kupigwa rusha roho. Lakini bado ina nafasi yake hii rusha roho. Ngoma hii ikiingia mtaani na hasa ikenda kule shamba, huwa wanakodiwa mjini wanakwenda zao shamba, huko wanajua sijui kama ndio chaka wanakwenda kujificha au vipi. Ngoma hii kwa kweli inavunja maadili sana. Watakuja pale shughulini, pataliwa karamu wakimaliza wao hawataki nyumba wanatafuta kichaka kidogo tu wanabadilisha nguo. Hapo, tena wanawake wanafika kupigana kisawa sawa mpaka vipaipu vya mfereji.

Kuna babu yangu mmoja anasema hii ngoma sio rusha roho, hii kidokoa roho. Ngoma hii nayo inamashaka yake, ningeliomba hii bodi ifanye utatifi wa kutosha. Kama kuna uwezekano hichi kibali kuzuiliwa, basi ingelizuiliwa maana ngoma hii katika hizo ngoma zisizovunjwa basi na moja wapo hii hata kuwe na adhana thelathini. Ngoma hii haisikii adhana, haisikii sala, wala haisikii chochote, wala hatokei mtu akenda akavunja pale, mpaka pale watakapoamua wenyewe kuvunja kama saa 2:00, saa 6:00 au saa 7:00 za usiku, itakapovunjika mpaka itamaliza muda waliojiwekea. Hii ndio hali tuliyokuwa nayo.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, pia tunataka uhakiki katika mikutano yetu ya kitaifa ya hadhara juu ya zile ngoma, kabla ya kupelekwa pale. Jana alisema mheshimiwa kwamba kuna mambo mazito huwezi ukamwambia Khadija Kopa hapo sipo usende. Ni kweli, lakini hapa panataka sisi wenyewe viongozi wa siasa tutumie nafasi hii kama zile. Siku moja kulionesha mkutano mmoja na wachukuaji wa TV nao kila wanapoona kwamba

hapa kuna mitihani ndipo wanapovuta hasa. Alivutwa mwanamke mpaka kumtazama huwezi, kuna kiongozi mmoja alikaa mdomo wazi saa nzima anatizama ile hali juu ya mwanamke jinsi anavyoadhirika uwanjani pale. Kama mimi ni mwanamke mwenzangu kumtazama siwezi je hao wanaume?

Haya ndio maadili tunayoyazungumza, mwanamke asifikie hatua hiyo, wewe mwanamke mwenzio basi unashindwa kutazama hali kama ile. Katika hadhara kama zile kunakuwa kuna mambo makubwa yanayotendeka katika mikutano. Kwa hivyo, na mule ningeomba katika fani zote mufanyiwe utafiti wa kutosha. Sio kwamba kenda kustareheshwa kiongozi basi. Kiongozi ndio wa kuheshimiwa, pale panatakiwa pawe na heshima ya juu kwa sababu watu wako mbele ya viongozi wao. Sio vyema wanawake waende wafanye mambo kama yule wa uwanjani. Haya mambo kama tutashirikiana kwa nia njema, kwa nia safi na sote tukiwa tupo kitu kimoja, basi nina imani hizi kelele zetu tunazipiga hapa zitapungua.

Wananchi wanatusikiliza, huku wakikaa wanasema wao kazi yao wakikaa kule wakapiga kelele basi, hakuna lolote linalofanyika. Hakuna lisilowezekana. Sasa hivi tuko mbali kwa hii hali jinsi ilivyopotea. Mila, silka, tamaduni zetu, tuko mbali nazo, tunawasi wasi kwa hatua iliyofikia hivi sasa tumeshaona kwamba ule wakati wa jihadi mtu kupigana na nafsi yake na angalau na familia yake umeshafika, na ndio wakati huu. Lakini tuko hatarini kwa mambo yaliyokuwepo katika nchi yetu ya Zanzibar hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu atunusuru kuja kutuletea mambo makubwa makubwa hili ndio la kuomba. Mwenyezi Mungu anasema hadhihirishi chochote katika ulimwengu ila maovu yatakapozidi katika nchi au katika ulimwengu. Tutakapopata majanga makubwa makubwa na leo hii tutizameni majanga ya ukimwi haya, ni kitu gani? Kutokana na kudhihirika mambo.

Kwa hivyo, huu ule wasi wasi wetu tukawa nao na tukajipanga basi *Inshaa Allah* Mwenyezi Mungu atatusaidia. Bodi nayo ifanye kazi zake kama ilivyotarajiwa. Haya mambo ya filamu ndio yanayopotosha watoto wetu, angalau yakawa yanapata unafuu kidogo, watoto wetu watapata kuweza kurudi kidogo katika nafasi zao. Heshima itarudi na watoto wetu watapata kusoma. Sasa hivi hakuna heshima kwa sababu kila kitu kipo nje mambo hadharani. Kila kitu mtoto keshakiona kwenye filamu, umwambie nini? Hunalo la kumwambia hata moja.

Mhe. Mwenyekiti, zamani wazee wetu wakati wa mama zetu na hadi sisi. Mama anakuambia kwenye unyago unapokwenda kuhadithia nje huko utakufa. Mtoto anakua anaogopa na anakuwa na hofu. Mtoto wa sasa umtishe nini? Anakwenda mpaka kwenye kaburi anachungulia mwanawa ndani. Sisi ilikuwa lile jeneza tukiliona tunakimbia. Kwa hivyo, ile hofu sasa hivi imeondoka hakuna hofu wala hakuna woga.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia hapo.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza nitakuomba sahamani kwani sitosimama. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa katika

Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima na salama *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tufanye shughuli hizi tukiondoka tukiwa tuko salama. Wale wenzetu wanaoumwa Mwenyezi Mungu awajaalie awape nafuu waweze kufanya shughuli zao, na wenzetu waliototangulia *inshaallah* Mwenyezi Mungu aziweke roho zao kuwa miongoni mwa waja wema.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati wa mswada huu nimeshapitia vifungu hadi vifungu na watu wameshachangia sana. Kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri, watendaji wake na wizara yake yote kwa kuweza kutuletea mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni mzuri na tumeuona na watu wameuchangia kwa kina. Azma ya mswada huu ni uhakiki uliotajwa hapa katika kanda za *video* na *CD*. Pia kuna yale malengo mengine kwani huu mswada umejibana lakini wakati kuna mila, desturi na mambo ya nchi hii lazima tutaingia huko. Hapo nitakapotoka nje naomba samahani.

Mhe. Mwenyekiti, mswada umeshachangiwa sana mimi nitagusia tu kidogo katika mswada huu wakati watu wameshauchangia katika mila na desturi za nchi yetu. Mhe. Spika, kuhakiki, kufanya sensa ya hizo kanda za *video* ni vizuri bodi ikajitahidi lakini hawatamaliza kazi yote, kazi nyengine zilizobakia za mila na desturi mheshimiwa na sisi wenyewe kwa sababu kuna chimbuko huku chini la watoto wetu ndio tunaowapigia kelele sasa hivi. Kwa hivyo, mimi nasema tujitahidi sisi walezi wa watoto hawa kwa sababu bodi sio kweli kwamba itafanya sensa na uhakiki ije mpaka majumbani kutufundishia watoto. Ninachosema ni kwamba tujitahidi sisi walezi hao bodi watafanya wanayoyaweza ila na sisi tujitahidi kurudisha silka, mila, heshima na utamaduni wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tunapata kuona mimi na mwenzangu malezi yetu tuliyolelea basi sio malezi tunayolea watoto wetu hivi sasa. Mapenzi ya watoto tumeyafanya mengi, huruma zimekuwa nyingi tunajilabu mtoto akifanya vibaya, lakini kwa hakika watoto wanapotoka na wazee tunaona. Mhe. Mwenyekiti, sisi tulipolelewa tulikuwa tunajua kuamkia huyu tumuamkie vipi, sasa hivi mtoto akikukuta wewe mtu mzima anakuuliza vipi mambo, hawezi kukuamkia shkamoo hilo hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, naomba mambo haya tujitahidi sisi walezi kuyaanza na ikisha wenzetu wa bodi watafanya kazi watakayopewa, lakini sisi hii mila na desturi tuanze sisi wazazi. Mimi nawalaumu sana wanaume kwani na wao watakwenda kuulizwa wamezichunga vipi familia zao. Mhe. Mwenyekiti, mwanamme amekumiliki anakwenda kukukatia kitambaa anachojua hiki wewe kinakufaa kushona kanzu na ikakuenea, unaichukua kanzu na pesa za kushonea anakupa. Unakwenda kwa mshoni kushona kanzu hiyo aina unayoitaka wewe. Kanzu hiyo ikija pengine ina mkono mmoja au pengine haina kabisa.

Pia unakwenda kwa mchoraji wa hina, kwanza hao wachoraji wa hina ninawaambia wanaume wanawajua huko *saloon.* Watu wanakwenda *saloon* kumbe wanaume ndio wanaofanya kazi hizo. Mimi nafsi yangu nimeshakwenda *saloon* mwanamme ndiye mpambaji. Mimi sijaona katika desturi yetu mwanamke kupambwa na mwanamme, labda mumeo ndani. Hivyo unakuja nayo kanzu unaivaa baba yupo anakuona na kitambaa

amekikata yeye kwa nini hapigi marukufu akakwambia uivue, pengine ndio anaona mke wangu leo ameshona kanzu nzuri mabega yako nje wala hujitandi mnatoka mnakwenda kutembea. Mhe. Mwenyekiti, haya yamo na tunayaona ndio tukaambiwa sisi tunaojitanda na kuvaa kanzu za mikono mirefu washamba. Lakini huu ushamba ndio mila na desturi zetu hayupo hata mmoja aliyezaliwa hapa mjini sote tunatoka huko shamba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa mtoto na atakayekuwa kiwango kama changu afahamu malezi hayo ya kuwa tunakulia mila na desturi mpaka tunapata ukubwa. Zile siku saba au kumi na nne za kuwekwa ndani humo mna mila na desturi tunafundishwa watoto wanawake wala hajui mtu nje nini tunafundishwa. Siku unayotoka huthubutu wewe kusema chochote maana ukitolewa siku ile nenda ukazungumze basi utakuja kuipata, huthubutu kuzungumza chochote na wala mwenzako hajui umefundishwa nini. Hiyo ndio mila na desturi yetu, mpaka utafika siku Mwenyezi Mungu atakayokujaalia kubahatika kupata mume basi ukihakikisha kwamba huyu ndiye anayekuja kuniposa mtu huyo ukimkuta njiani unamkimbia hamuonani mpaka itafika siku ya harusi. Mhe. Mwenyekiti, mtu huyo huyo siku ya harusi kuna saba moja wewe unawekwa ndani unakabidhiwa mtu anakutia hina ndani, hina haionekani mpaka siku utakayoolewa aje aione bwana harusi. Kuna siku saba nyengine umeshaolewa unawekwa ndani za kukaa na bwana tu mpaka zinamalizika. Hiyo ndio mila na desturi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano leo Bi Raya nafanya harusi ya mtoto wangu eti, najilabu nakuja kutafuta nguo nzuri ikisha mtoto yule kuanzia Chake-Chake, Wete kote huko hakuna mpambaji namtia kwenye ndege anakuja kupambwa Unguja au Dar es Salaam. Mhe. Mwenyekiti, pengine chakula huna lakini pesa za kumchukua mtoto yule kuja kupambwa huku unayo. Unakuja kumkabidhi watu achorwe hina na apambwe na wanaume ndio wanaozifanya kazi hizo. Mimi mwenyewe nimekwenda *saloon* Dar es Salaam nimeshuhudia mwanamme anamchora mwanamke hina kuanzia kisugudi mpaka tumbo na kuanzia mkono mpaka kifua. Je, hizo ndio mila zetu na desturi? Mhe. Mwenyekiti, tayari Zanzibar pia jambo hilo limeshafika hapa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, pengine mimi na baba tunashadidia kwenda kukodi ukumbi, tunamchukua mtoto tunakwenda naye kwenye *hall* tunamuweka mtoto pale amevaa kanzu mkono mmoja au pengine iko kifuani anaonesha hina. Mume anakuja pale anaingia anafika anakumbatia mke wake mambo yote yaliyokuwa ni ya siri yanafanyika hadharani, hivyo tunafanya nini. Sisi wenyewe tusije kuilamu bodi, bodi kweli itapewa kazi yake ya kufanya sensa lakini jamani sisi wenyewe ndio turudishe mila majumbani bila ya kufanya hivyo mheshimiwa maadili hayawezekani yataporomoka yamung’unyike kwa sababu tunayachangia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, baba ndani anakuja anamuona mtoto imeshafika wakati wa sala kila kitu anakuachia wewe mama, sisi tutafanya mangapi. Mama aende shamba, alee mtoto, huku mjamzito, atafute maji Mhe. Mansour Yussuf Himid maji miezi mitatu hatupati yeye anataka tulipe tu na ikisha hapo hapo mimi aniachie watoto niwaambie wakasali, wafue nguo na kila kazi. Hilo haliwezekani wanaume warudishe silka zetu. Mtoto mwanamme ikifika wakati wa sala basi baba yake amchukue amwambie twende

msikitini, na mtoto mwanamke aachiwe mama afundishwe tusije tukailaumu hii bodi hawa wana jambo moja tu la kuhakiki kinachoingia na kinachotoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshuhudia kwa jicho langu kanda ya harusi mtoto wako wewe mwenyewe hina unamualikia watu zaidi ya mia mbili na wanaume wanakuja na *video* kuja kumchukua. Mapaja yanakuwa nje, kifua nje na kanda hizo hizo watu wanarushiana zinauzwa na tunaziona. Kwa hivyo, mimi naona tuna kazi refu wazazi kwa sababu zamani silka na mila zetu tulikuwa tunalelewa na jamii yote. Kwa mfano, mimi nikikutwa nimefanya kosa basi atanikamata mtu anipige na ikisha mzee wangu hasemi kitu. Lakini leo huthubutu mtoto wa mwenzako kumrudi neno.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwalimu wa chuoni basi niliposomesha zamani sio hivi sasa. Hivi sasa mimi nimeshasomesha na tayari nimeshamrudi mtoto na nikaekewa vikwazo juu ya mtoto huyo. Mtoto huyo alitolewa chuoni kwangu akapelekwa chuo chengine laana ya Mwenyezi Mungu nayo sio ndogo, kwani mwenye kukuanzisha ile herufi moja tu basi ni mwalimu wako, basi Mwenyezi Mungu alimpiga laana juzuu zile zile nne alizosoma kwangu hakusoma tena. Mimi nilishukuru bora Mwenyezi Mungu alinifanyia lenye kheri. Lakini sasa hivi hakuna kumrudi mtoto wa mwenzako ila ujitahidi wewe mwenyewe ndani kwa sababu tunayaondoa yale maadili kuwa mtoto wangu mimi asifundishwe na mwenzangu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mapenzi yatatuweka pabaya ya watoto, kwani tunawapenda sana watoto na kuacha mila zetu na desturi ndio watoto wakafanya mambo yaliyokuwa hayastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ya kanda yapo, lakini kuna na mambo mengine huko vijijini watu hawana kanda wala hizo televisheni zilikuwa hakuna. Watu walikuwa wanafanya mambo yaliyokuwa hayastahiki. Watoto wanalewa, watoto wanafanya mambo ya uzinifu, wanafanya mambo machafu huko maskulini ndio kabisa. Kwa hivyo, mimi naomba katika mswada huu wa uhakiki wenzetu hawa wa bodi watakuwa na mzigo mkubwa wa kuhakiki kanda zitakazoingia lakini na sisi hii mila na desturi tusiipoteze.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba hii mila na desturi tuanze kuwafundisha watoto wetu majumbani desturi zetu, silka zetu na mila zetu hapa Mwenyezi Mungu labda anaweza akatusaidia kidogo tukapata nafuu. Lakini kwa kusema madhali huko kumeshawekwa bodi inahakiki kila kitu, kweli hii itakwenda ihakiki kinachoingia kwenye nchi na ikisha tuje huku majumbani watu wanafanya nini. Hilo haliwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, nasema sisi wenyewe watoto tunawapalilia kwani watoto Mwenyezi Mungu amewajaalia wana hikma kushinda sisi tunaofika miaka mia, watoto wanatakiwa watizame televisheni mpaka itafika saa mbili au saa tatu wanachawanyika. Mimi nimeshakwenda pahali na nikawakuta watoto wanakanda wanatizama na ndani watu walikuwa wameshalala nimeshtuka nakuta TV iko wazi. Nikauliza kuna nini huko? Nikafungua pazia nikachungulia kumbe walikuwa wanatizama hizi kanda za mambo ya watu wazima. Mhe. Mwenyekiti, hiyo sio kanda ya kutizama mtoto wala wewe baba mtoto na mama mtoto sio kanda za kutizama. Wewe ni mtu mzima mwanamke umeshaolewa, mwanamme umeshaoa kuna la ajabu gani unalolitizama kule, silioni ila

nikujikashifu wewe mwenyewe kwa sababu kile kitendo kinachofanywa sio kigeni kwako.

Kwa hivyo, mimi naomba hizi kanda nyengine zitakapohakikiwa zipigwe marufuku kabisa zisiwepo ziachwe na hizi laana zao nyengine ndogo ndogo maana sio kweli kwamba haya kwa leo na kesho kama tutayaweza, haya hatuyawezi, ila tujitahidi na Mwenyezi Mungu atatusaidia. Watu walisema kwenye shida kubwa basi kutakuja raha kubwa na *inshaallah* Mwenyezi Mungu ameshatuanzia hili basi ataweza kutujaalia tukayamudu mambo hayo, ila nasema wazazi tuna kazi kubwa juu ya watoto tusikubali.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja naondoka narudi kwangu, watu wameshanidai pesa za suruali na pesa za kununulia mkanda, nikaweka pesa hizo kwani ilikuwa karibu ya sikukuu watu wakaenda wakajilabu mimi nikirudi nyumbani na mitandio yangu nimechoka naingia nakulala tu. Baada ya kurudi huku Unguja nimeshafika pale nyumbani watoto wanakuja kuniamkia kuna mtoto wangu wa mwisho na mtoto mwengine namlea mle ndani. Kwanza waliponiona wakanipita bila ya kuniuliza chochote, nimetulia natizama nasema na roho yangu leo kulikoni, ikisha akapita na yule mwengine ndio hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kumbe watu wamevaa suruali zao nzuri lakini ukanda uko chini. Nikasema nasubiri wanipitie tena mara ya pili hapa basi watahama au nitaambiwa nihame mimi mama. Basi kwa bahati akapita tena yule mtoto wangu asipite yule wa mwenzangu, nikamuuliza haya ilikuwaje. Akaniambia kwani nimefanya nini? Nikamuuliza suruali ndio inavyovaliwa hivyo naona leo mkanda uko chini, nasema ikavuliwe au mkanda uvue. Pale pale aliingia ndani na suruali akaivaa vizuri na mpaka leo hathubuti kunipitia na yule mwenzake alikwenda kumwambia kwamba vaa mkanda vizuri Bi Raya yuko huko ameshakuja hana ila kero. Lakini mambo ya kuvaa suruali ukateremsha mkanda chini ya makalio kwangu mimi isivaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, ningenyamaza kimya basi siku ya pili ingevuliwa kabisa akanijia na chupi, nikamwambia hapa usipite, mwanamme hana wakati, mwanamme saa zote yeye amejitwika mara kaenda kuchunga ng’ombe una kazi gani usikae nyumbani ukamsaidia mwanamke kulea watoto. Mimi nasema wanaume msitubwagie ulezi peke yetu halafu mkasema watoto majumbani wanaharibika, maadili yanamong’onyoka. Kwa kweli mheshimiwa wanaume hawataki kulea watoto wao kila mmoja amejitia suti yake anazinga mwanamke mwengine anakwenda kumuoa, lakini huku nyumbani unaachiwa peke yako ulee watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema maadili bila ya kuweza kuweka ushirikiano baba na mama ndani yatamong’onyoka na hatuyawezi, watoto tuwapige nguvu tusishindwe na tunachokizaa mtu haogopi mtoto wake japo atakutukana lakini wewe sema tu kwa sababu huu umri Mwenyezi Mungu ameshauweka kuwa mtoto awe juu kuliko baba na mama. Lakini tusiwe hivyo tuseme kwani tutakaposema Mwenyezi Mungu atatupa nguvu watoto wanafanya mambo yaliyokuwa hayastahiki. Kwanza unalala vipi mtoto yuko nje saa sita za usiku hajaja ndani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mwenyezi Mungu amenipa watoto wawili tu wanaume, lakini bila ya kujua mimi kwamba watu wamesharudi kusali sala ya Isha wanakuja ndani kulala basi mimi silali. Kwanza ninachokihofia kupita mitaani kumeshazuka balaa nikaja kuambiwa mtoto wangu ndiye aliyezua balaa, basi humwambia kaa humu ndani likuzukie balaa tumo humu humu. Ikiwa ni TV ndani imo tizama pale sitaki kwenda kutizama katika nyumba ya mtu. Kwa hivyo, naomba tujitahidini na televisheni tusiwaekee na hizo *video* kwani ni kwenda tukatafuta mambo tukawatilia watoto sisi hatutizami wakati hatuna lakini wao wanaona mambo mengine mazito. Siku moja tuliambiwa hapa patakuja chombo cha kudhibiti hivyo tunaomba kije haraka kwa sababu michezo mingi sana iliyokuwa imo katika televisheni zetu ni michezo mibaya.

Jana tu hapa unajadiliwa mswada huu huu basi tumekwenda hapo ukumbini na waheshimiwa wenzangu tumeona kwenye TV bibi na bwana wanafanya mambo yao hadharani. Sasa pahala kama hapo pakiwa pana watoto mtatizamana vipi. Kwa hivyo, tunaomba hizi kanda zitakazohakikiwa bodi wahakikishe kwamba kanda zilizokuwa hazifai nchi hii ziondolewe kabisa kwani sio maadili yetu. Sisi tuna maadili yetu ya Kizanzibari taarab na ngoma nyengine na mafunzo mengine hatuwakatazi watu kutazama michezo yao lakini waweke wakati maalum kwani yanaharibu maadili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mtoto wa miaka miwili akija hapo akijifunga kibwebwe akicheza kiuno basi mtu mzima wa miaka mia hajui, ilikuwaje na hajafundishwa na mtu. Lakini ni kwamba ameona kwenye televisheni ndio anaiga. Siku moja tumo kwenye meli tunasafiri na *Sea Express* mimi na mke wa shemeji yangu yeye amemchukua mtoto wake tunatoka Dar es Salaam. Mhe. Mwenyekiti, tulikuja zetu mpaka tukafika Unguja tukaunganisha mpaka Pemba. Mimi nilikaa kiti cha nyuma wao wakakaa kiti cha mbele basi hapo ilioneshwa kanda sikufichi, mimi huku kwenye kiti nilizama nikatulia kumbe huyu mwenzangu amelala lakini yule mtoto yuko macho. Hapo yalifanyika mambo hata yalipokwishamaliza basi alimuamsha yule mama yake akamwambia hebu amka wewe mtizame yule mwenzako anavyomkosha baba, mambo yalikuwa yameshamaliza watu ndio wanakogeshana. Mhe. Mwenyekiti, tuliinama sote kwenye meli kila mmoja anaona tabu kumuangalia mwenzake.

Mhe. Mwenyekiti, kanda zitakazohakikiwa iwe ni sehemu zote ikiwa kwenye meli, ikiwa kwenye vilabu wahakikishe kanda kama hizo zipigwe marufuku. Tunaomba bodi hii Mwenyezi Mungu aijaalie iundwe, wizara pia Mwenyezi Mungu aipe nguvu na *inshaallah* wakati imeshatia nia basi itapata nguvu ili mambo haya yote waweze kuyadhibiti na Mwenyezi Mungu atujaalie na sisi wazazi atupe roho za imani kuweza kuwakataza watoto wetu machafu ili tupate kile tunachokihitajia.

Mhe. Mwenyekiti, namnpongeza sana Mhe. Waziri na nauunga mkono mswada huu mia kwa mia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa bodi ya sensa. Pili naomba nimshukuru Mhe. Waziri Kiongozi, Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na viongozi wote kwa kutuongoza. Tatu naomba

nitoe pole kwa familia ya marehemu Mhe. Daud Hassan Daud ambaye ametutoka hayupo na sisi leo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie mswada huu moja kwa moja. Kwanza kabisa naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Raya Suleiman Hamad kwa kweli mheshimiwa huyu ameufahamu huu mswada kwa undani maana ile tafsiri ya kuzuia kila kinachoingia na kinachotoka ameeleza kwa uhalisi wake. Pili naomba nitoe ushauri kwa watendaji wa bodi ya sensa ambao wako karibu sana pale wamekaa na Bi Raya tuna haja ya kuchukua semina kutoka kwa Bi Raya kwa sababu leo amefafanua mswada huu wa sheria kwa undani wake na kwa uhalisia wake.

Kwa hivyo, tuna haja ya kuchukua semina na mimi mwenyewe nitakuja kwako kwa ajili ya semina ili unifunze mengi zaidi. Tatu kwa heshima na taadhima nitamuomba Mhe. Waziri wa Habari na Michezo pale ambapo sheria hii ikishapitishwa na kusainiwa basi mjumbe mmoja wa bodi ambaye mimi binafsi nitamuomba yeye Mhe. Waziri akuchague ni wewe Bi Raya. Hilo naliweka wazi hapa na Mhe. Waziri wangu bahati nzuri yupo na analisikia hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nijaribu kuchangia katika mambo mbali mbali ambayo yalizungumzwa na waheshimiwa mbali mbali. Nikianza na mwenyekiti yeye alitoa hoja moja katika maelezo yake kwamba kuna manispaa inatoa kibali cha matangazo yanayowekwa barabarani, lakini wakati huo huo bodi ya sensa nayo inatoa kibali kwa tangazo lile. Sasa kazi ya manispaa ni kutoa nafasi ya lile tangazo la kutolewa pale barabarani, lakini kazi ya bodi ya sensa ni kutazama kile kilichokuwemo ndani. Mara nyingi utakuta matangazo ya biashara hata kule Tanzania Bara hasa haya makampuni ya simu wanaweka picha nyengine ambazo ni kinyume na silka, utamaduni, na maadili ya Mzanzibari. Kwa hivyo, vibali hivyo vitatoka upande wa manispaa watatoa cha kwao na upande wa bodi ya sensa pia itakuwa inatoa kibali chake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Abdalla Ali yeye alitaka zaidi ufafanuzi wa neno mazingaumbwe lakini naomba nieleze kwamba mazingaumbwe ni mbinu za kiufundi, usanii na ujanja zinazotumiwa na baadhi ya watu katika kuwaghilibu wengine kwa misingi ya kuburudisha ili waamini kile wanachokiona japokuwa sicho. Katika sheria ile ya Kiingereza mazingaumbwe ni *magic show* na tafsiri ya uchawi ni *witchcraft* kwa hiyo hii ni *magic show* na ndio tafsiri iliyokusudiwa katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na hoja ya Mhe. Ali Abdalla Ali ukurasa wa 228 *paragraph* ya 10 ameeleza tafsiri ya nyumba ya burudani. Nyumba ya burudani imetajwa katika tafsiri hii na iko wazi kabisa kwa hiyo naomba nimuhakikishie kwamba ukumbi kama wa *Salama Hall* ukitumika kwa hadhara ya burudani kama hiyo nao pia utaingia kwenye tafsiri hii hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia kuna hoja ambayo ilitolewa na Mhe. Ali Abdalla Ali kwamba mambo haya sio hadharani tu, lakini namshukuru Mhe. Haji Faki Shaali alilijibu hili kidogo kwamba tusinyime uhuru wa mtu kwa kusema kwamba hata pale *private* anapofanya ambapo sio hadharani sheria hii isimguse. Sheria hii inagusa

mambo mengi ambayo yako hadharani bila ya kunyima uhuru wa mtu. Kuna michezo ambayo ni ya kuigiza ambayo haitumii maneno, hiyo michezo ipo na watu wanafahamu kwa vitendo na Mhe. Ali Suleiman Ali alieleza hapa michezo ya kule Rwanda alipokwenda aliona watu walikuwa wakitikisana mikono na walikuwa wakifahamika vizuri.

Pia kuna hoja iliyotolewa ya kuanzishwa Chuo cha Utamaduni na Sanaa hili naamini Mhe. Waziri mwenyewe analisimamia na ni hoja nzuri sana ambayo sote kwa pamoja tunaiunga mkono na tunaamini siku moja tutakuwa na Chuo chetu wenyewe cha Sanaa hapa Zanzibar. Alizungumzia suala la mganga wa kienyeji kuwa na kibanda kibovu, amevaa kaniki na kadhalika. Hata katika michezo ya kuigiza huwa wanaigiza namna hiyo na wenzetu wa Nigeria huwa wanaigiza mganga wa kienyeji amevaa suti. Lakini kwa hapa kwetu kwa utamaduni wetu na tulivyozoea basi mganga wa kienyeji mara nyingi hicho ndio kivazi chake na ndio maana hata hao waigizaji katika hayo maigizo wanatoa sifa hiyo kwa mganga wa kienyeji.

Mhe. Salmin Awadh yeye zaidi alizungumzia ngoma za asili kufufuliwa na leo kuna ngoma za kisasa nyingi kama vile rusharoho na nyenginezo. Lakini kuna idara ambayo inashughulikia suala hilo la kufufuliwa kwa ngoma za asili ambayo ni Baraza la Sanaa. Hii Bodi ya Sensa kazi yao hasa ni kusimamia kile kinachokwenda kuoneshwa lakini Baraza la Sanaa lina jukumu la kusimamia utamaduni na asili ya Mzanzibari pamoja na ngoma zake na mambo mengine yote ambayo yanahusiana na hayo.

Vile vile ameuliza kwamba mswada huu utakuwa na uwezo wa kusimamia majumba ya sinema? Mswada huu utakuwa na uwezo kikamilifu kusimamia majumba ya sinema na baada ya kupitishwa watajengewa uwezo ambapo wataweza kusimamia masuala kama hayo yanayohusiana na filamu ambazo zinaoneshwa kwenye sinema.

Ushauri wa kuwashirikisha *NGO’s* kama *spirit* ile ya *private partnership* ya kuwa nao katika bodi hili, naona hatutakiwi tum-*limit* Mhe. Waziri katika kuchagua bodi yake, tunatakiwa tumpe uhuru. Lakini naamini Mhe. Waziri wakati anachagua bodi yake atakuwa anaangalia pia sekta binafsi ili wao waweze kushiriki katika kufanya kazi nzima ya Bodi ya Sensa.

Alizungumzia pia kuhusu mabango ya biashara na sio taarifa za utangazaji. Bodi ya Sensa itashughulikia zaidi yale mabango ya biashara na sio taarifa za utangazaji kama lile bango la *TRA*, lile halihusiani zaidi na Bodi ya Sensa, vyenginevyo labda kama kuna lugha itakayotumika kinyume na silka na mila. Kwa mfano, nitatoa neno moja ambalo linatumika kule Tanzania Bara ambapo hapa Zanzibar halitumiki na kuna neno linatumika hapa Zanzibar na Tanzania Bara wanalikwepa sana kulitumia. Neno ’kusimikwa’ linatumika sana Tanzania Bara lakini haba Zanzibar neno hilo halitumiki na neno ’kutawazwa’ linatumika hapa Zanzibar ambapo Bara kidogo wanalikwepa. Kwa hivyo, katika lugha Bodi ya Sensa pia itakuwa na uhakiki wa lugha ambapo suala hili pia lilitajwa na Mhe. Zakiya Omar Juma.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla yeye alizungumzia zaidi kivazi cha mila ya Mzanzibari na akatoa mfano wa Chuo cha Kiislamu. Mfano wa Marehemu aliyekuwa Kadhi Mkuu wetu Mussa Makungu pamoja na yule Mama wa Kiingereza. Nchi nyingi katika mila na silka na katika sheria zao wanaweka hilo. Mfano mzuri nitatoa nchi ya Iran.

Nchi ya Iran wao kwa mgeni yeyote anayekwenda, mle ndani ya ndege yao basi wanatoa mtandio kama wanavyogawa chakula basi huwa wanatoa mtandio kwa mwanamke ili kabla hajashuka kwenye uwanja wa ndege awe ameshajitanda kichwa chake. Hiyo ni sheria kwa nchi ya Iran. Kwa hivyo, mimi naomba nikubaliane na wewe na kuchukua ushauri wako kwamba kuna mila, desturi na silka za Mzanzibari hizo lazima zifuatwe na bila shaka kuna Dini pia ndani ya mila na utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Mohammed Ali Salim yeye alizungumzia zaidi kwenye masuala ya teknolojia. Naomba nimpongeze sana Mhe. Rashid Seif kwa sababu kutokana na takwimu za Baraza la Wawakilishi yeye ni mtumiaji mkubwa sana wa hizi kompyuta zetu hapo juu *internet cafe* iliyoko juu. Sijajua bado anatumia kwa shughuli gani au anaangalia nini lakini nataka kusema kwamba kwenye masuala ya *internet* mambo mengi yanapatikana. Wenye kwenda kutafuta *Kur-ani* wanapata humo humo, wenye kutafuta tafsiri ya *Kur-ani* wanapata humo humo.

Mimi juzi nilikuwa najaribu kutafuta baadhi ya aya za *Kur-ani* kwa sababu siku hizi kuna *search engine* moja ya Kiislamu ambayo unaweza kutafuta aya moja kwa moja inayohusiana na jambo fulani, aya zenye kuhusiana na ndoa unaweza kuzitafuta moja kwa moja kwenye *internet*. Lakini wakati huo huo *internet* hiyo hiyo ina mambo mengine ambayo ni kinyume na mila zetu na silka. Nchi nyingi duniani zinajaribu sasa hivi kuzuia, moja wapo ikiwa ni Saudi Arabia, Iran pamoja na nchi nyengine, lakini kwa kuwa ile *technology* haikuanzia kwao na iko kwengine basi inakuwa vigumu sana kuzuia vitu vyote. Kwa hivyo, uwezo huo na nguvu hizo itakuwa ni vigumu sana kwa nchi changa kama ya kwetu kwenye teknolojia kuweza kuzuia.

Nchi zilizoendelea basi wanahangaika sana kuzuia masuala hayo na bado kila siku wale watundu wa *internet* wanapata upenyo wa kutuma vitu vyao kwa njia nyengine. Haya pia kwenye simu kwa sababu siku hizi mtu unaweza kukaa hapo Mhe. Mohammed Ali Salim na mimi niko hapa naweza nikakutumia kitu katika simu yako ukiwasha na ukitizama utakuta ni nje ya mila na silka lakini ni teknolojia ambayo inaendelea. Lakini wakati huo huo pia naweza nikakutumia aya ya Kur-ani. Kwa hivyo, ni jukumu letu sisi kama alivyosema Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak kuwa ni jukumu letu sisi kuelimisha jamii kama Bi. Raya Suleiman Hamad alivyohangaika kuwaelimisha watoto wake kuwaambia kipi sahihi na kipi si sahihi. Kuvaa suruali na nguo ya ndani ikawa juu sio sahihi ni jukumu letu sisi kutumia zile teknolojia zilizokuwepo kwa njia iliyo sahihi na sio kinyume na hapo. Lakini kusema unafunga kabisa ni tabu, hata hao Wamarekani wenyewe ambao *internet* iko kwao zaidi kuliko nchi yoyote nyengine bado hawajafikia kiwango hicho juu ya kuwa na vifaa vyote lakini bado hawajafikia huko.

Mhe. Mohammed Ali Salim pia aligusia sifa za Mwenyekiti. Mimi maoni yangu hapa kwenye sifa za mwenyekiti tusim-*limit* Mhe. Rais katika kuchagua mwenyekiti. Kwa

sababu tukisema awe na sifa zinazohusiana na utamaduni au sifa kadhaa, kwa kweli katika michango iliyotolewa hapa Mhe. Mula ametoa mchango mzuri sana, Mhe. Haji Faki Shaali tangu tulipokuwa naye kwenye kamati ametoa mchango mzuri sana. Sasa leo kama Mhe. Rais anataka kuwachagua nyinyi mmoja wapo kuwa mwenyekiti, natoa mfano wakati huo huo huna sifa ambazo zinazohusiana na utamaduni, ikiingizwa hapa kwa kweli hata wewe mwenyewe unajipunguzia nafasi yako ya kuchaguliwa. Ninachotaka kusema kwamba nafasi ya kuchaguliwa bila shaka Rais ana hekma na busara ambazo atatumia nafasi hiyo kumchagua mtu mwenye uzoefu na uelewa wa utamaduni, mila na silka za Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja ya Mhe. Ame Mati Wadi aliyoisema kwamba ulezi ni wetu sote yaani huu ulezi wa utamaduni ni wetu sote. Mimi naungana mkono naye asilimia mia juu ya mia katika hiyo kwa sababu hili ni jukumu la wote.

Katika hoja zake nyengine Mhe. Ame Mati Wadi pamoja na Mhe. Rashid Seif Suleiman pamoja na Bi. Raya walizungumzia kwamba bado kuna *video* na *DVD* na mambo mengine zinauzwa njiani. Hizo mkipata taarifa Bodi ya Sensa ipo tuleteeni taarifa. Lakini naomba nieleze hivi, katika ile *survey* tuliyoifanya ya habari hapa Zanzibar bado maadili, mila, silka za hapa Zanzibar zimeonekana ziko juu zaidi kuliko wenzetu Tanzania Bara. Kwa sababu zile *DVD* kwa wenzetu Tanzania Bara kule unakuta mtu kabeba *CD* nyingi njiani lakini ya mwanzo na ya mwisho huku ndio hizi filamu za kawaida tunazotizama za kati kati zote sizo, huwa anakuja pembeni kwenye gari anakuonesha na kukuuliza mzee vipi unataka? Kwa hivyo, kule zimesambaa zaidi kuliko hapa. Sasa sheria hii ikipitishwa itawapa meno Bodi ya Sensa kuweza kutafuna na kuzuia masuala kama haya. Kwa hivyo, bado naweza kusema kwamba sisi tuko katika hali nzuri kuliko wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuna hili neno sensa na uhakiki limezungumziwa sana. Lakini ninachotaka kusema neno sensa tukilitafsiri hasa katika upana wake ni pana sana na linajumuisha mambo mengi. Lakini tukija kwenye uhakiki tutakuwa tunagusa jambo moja tu. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana na niombe hata kwa Mhe. Waziri libakie neno hili wakati anakuja kujumuisha ili twende nalo badala ya kuingia kwenye uhakiki kwa sababu uhakiki unatu-*limit* na una-*limit* nafasi na nguvu za Bodi ya Sensa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Zakiya Omar Juma alizungumzia kuhusiana na kuporomoka kwa mila, desturi za Mzanzibari na vile vitabu vya zamani virudishwe ambavyo vinamfunza Mzanzibari utamaduni, mila na silka. Ushauri huo tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Pia alizungumzia masuala ya uhakiki wa lugha nao pia utizamwe. Kiswahili kinachotumika nacho kiwe *censored* katika kazi ya Bodi ya Sensa. Naamini Bodi ya Sensa itafanya hivyo itakuwa na mtaalamu wa lugha ya Kiswahili . Sasa hivi baadhi ya watendaji ni wataalamu pia wa lugha ya Kiswahili na naungana naye mkono asilimia mia juu ya mia kwamba wale wanaopewa vibali bahati mbaya sio Bodi ya Sensa wanaotoa vibali vya kupiga ngoma yale magari makubwa ya *Vodacom* na *Zain* na wengineo. Naungana naye mkono kwamba vile vibali vitolewe kwa muda maalum na wakati wa adhana ni marufuku kupiga ngoma hizo, hiyo ni mila, utamaduni na silka ya Mzanzibari.

Kwa hivyo, naungana naye kwamba hilo litapigwa marufuku tutalishughulikia na ni Baraza la Sanaa ambalo linashughulika na masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba na mimi niseme kwamba mswada huu ni wa kitaalamu zaidi, mswada huu unahusisha mambo ya filamu na sanaa. Mhe. Ame Mati alitaja sanaa ya uchongaji ambayo pia inamuathiri katika jimbo lake kule kwenye sekta ya utalii. Naomba niseme kwamba haya yote baada ya sheria hii kupitishwa rasmi basi yatatupa nguvu sisi kama wizara itaipa nguvu Bodi ya Sensa, itaipa nguvu wajumbe wake pamoja na yule niliyemuombea Mwenyezi Mungu alijaalie atafanikiwa ili iweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi na wananchi wenzangu wa Jimbo la Mpendae tunaunga mkono mswada huu asilimia mia juu ya mia, tunaomba muupitishe ili tuweze kuufanyia kazi na Bodi ya Sensa ianze kazi yake mara moja kutokana na maoni yaliyotolewa ndani ya Baraza lako tukufu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuja kutoa majumuisho mswada ambao niliuwasilisha jana.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa nikiwa mzima na mwenye afya. Pili nawashukuru wachangiaji wote waliochangia mswada huu nao jumla yao ni Waheshimiwa 17. Naomba niwataje mmoja baada ya mwengine kwa kuwapa heshima zao.

1. Mhe. Ali suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii)
2. Mhe. Najma Khalfan Juma (Waziri Kivuli/Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo)
3. Mhe. Ali Abdalla Ali
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
6. Mhe. Mohammed Ali Salim
7. Mhe. Ame Mati Wadi
8. Mhe. Rashid Seif Suleiman
9. Mhe. Zakiya Omar Juma
10. Mhe. Haji Faki Shaali
11. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
12. Mhe. Ali Denge Makame
13. Mhe. Said Ali Mbarouk
14. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi
15. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
16. Mhe. Raya Suleiman Hamad
17. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo

Waheshimiwa wote waliochangia nawapongeza sana na nawashukuru kwa michango yao na wengi michango yao wameelekeza katika kutoa ushauri zaidi lakini pia katika

kuongezea maelezo ya hapa na pale katika vifungu vilivyotajwa, kwa lugha nyengine kuuboresha mswada huu ili bodi itakapochaguliwa iwe na nguvu na iweze kutekeleza kwa kiwango kile ambacho kinaweza kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, pili nataka nianze kwa kutoa tafsiri ya mambo mawili matatu ambayo Waheshimiwa walikuwa wanayauliza na kutaka ufafanuzi wa mambo hayo. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya mwaka 2004. Hii ni *second edition* kwa hali yoyote ni ya karibuni sana na imekuwa *re-printed* mwaka 2005. Nachagua yale maneno kama matano ambayo yaliulizwa sana kutakiwa ufafanuzi au tafsiri na mengine Mhe. Naibu Waziri wangu ameshayatolea tafsiri na ufafanuzi.

Kulikuwa kuna swali burudani maana yake nini? Kwa mujibu wa tafsiri hii inasema shughuli au kitendo kinachofanywa kwa ajili ya kufurahisha na kuchangamsha watu au kwa tafsiri nyengine ndogo tu inasema burudani maana yake ni sherehe.

Neno filamu. Mhe. Mwenyekiti, tukubali kwamba kuna maneno mengine katika lugha yetu ya Kiswahili yameazimwa, kwa lugha ya siku hizi wanasema yametoholewa kutoka kwenye lugha nyengine. Kiswahili chetu kimekusanya maneno mengi ya namna hiyo kama vile ya Kiarabu, Kijerumani lakini maneno ya Kiingereza pia yako mengi yaliyotoholewa. Kwa hivyo, hapa katika kulitohowa neno *film* la Kiingereza linaitwa filamu na kwa sababu limezoeleka kutumika linakubalika kutumika hivyo. Sasa tafsiri yake ni neno lililotoholewa kutoka neno la Kizungu *film*, maana yake ni ukanda wa aina ya *plastic* au aina nyengine ya kisasa ambayo hutumika kupigiwa picha ya *camera* na hiyo *camera* nayo imetoholewa, maonesho ya sinema au picha. Hiyo ndio maana ya neno filamu.

Mazingaombwe Mhe. Naibu Waziri amelitolea ufafanuzi. Kutokana na kamusi hili mazingaombwe maana yake ni kiini macho, mazingara; kuna mazingira na mazingara hapa ni mazingara, mambo ya uchawi na kadhalika ndio mazingaombwe hayo.

Kuhakiki, hili ni rahisi ni kutaka uhakika au kutafuta uhakika wa jambo ambalo linahitaji maamuzi au utekelezaji na kadhalika.

Mwisho neno bodi nalo limetoholewa kutoka lugha ya Kiingereza *board* na kwa lugha ya haraka haraka bodi maana yake ni halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo kwanza nije kwa majibu ya jumla kwa yale maeneo ambayo Waheshimiwa wengi wameyachangia.

Suala lililojitokeza sana na wengi wamelichangia ni kuweka sifa za mwenyekiti. Mimi kwa hekma ya Naibu Waziri alivyoeleza nakubaliana nayo. Kwa mfano, Mhe. Naibu Waziri amemtaja Mhe. Mohammed Ali Salim kwamba amechangia vizuri, mimi nilikuwepo nimemsikiliza ni kweli amechangia vizuri. Amemtaja Mhe. Haji Faki Shaali, hapa sikuwepo lakini kwenye kamati amechangia vizuri na amesaidia sana, ana upeo na uwezo mkubwa katika masuala haya lakini pia nimeshuhudia michango ya Mhe. Raya Suleiman Hamad.

Sasa Mhe. Naibu Waziri amependekeza kwamba nitapokuwa nachagua wajumbe wapya wa bodi baada ya sheria hii kupitishwa alipendekeza Bi. Raya nimchague. Pendekezo lake naliunga mkono na kwa sababu hata kama mimi ndiye mwenye mamlaka ya kuchagua lakini yeye anajua kwamba tunachagua kwa pamoja na kwa hivyo tunaoshirikiana wote wapo hapa na wamesikia. Mimi nawashawishi kwamba Bi. Raya anaweza kuwa Mwenyekiti wa Bodi kama wajumbe hawatasisitiza kuwa Mwenyekiti wa Bodi lazima awe na cheo, awe na *qualification*, awe na *degree* au *diploma*.

Kama alivyoshauri Mhe. Naibu Waziri tumuache Mhe. Rais upeo wake wa kufikiri na yeye Mhe. Rais huwa anawauliza watu na kutaka maoni kwa watu na kwa kawaida yake nina hakika kwa asilimia 80 amesikia mchango wa Bi. Raya leo.

Kama hakuusikia nitajitahidi ili ausikie huenda katika majina matatu nitakayoyapeleka moja likawemo pengine akaamua kumchagua. Kwa hivyo, nakubaliana kabisa na wazo la Mheshimiwa tujikite katika *qualification*, tukiliacha wazi tutapata upeo mkubwa wa kumshauri Rais ipasavyo kumchagua mwenyekiti, tukibakia kwenye *qualification* tutakuwa tunamfunga kidogo Mhe. Rais. Kwa hili hata kama ni la kitaalamu lakini si la kitaalamu kwa lugha nyengine hili *technical*, kitaalamu kwa maana ya kuweza kuwa na uwezo, juhudi, fikra, uzoefu wa kusimamia hayo yote mliotushauri na mlioyasema.

Waliozungumza haya ya mwenyekiti awe na taaluma ni Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Mohammed Ali Salim na Mhe. Rashid Seif, hawa ndio waliochangia. Kwa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri na maelezo ninayoyatoa sasa hivi pamoja na kuheshimu michango yao lakini nadhani tukubaliane iwe hivi tunavyoshauri kama ilivyo katika mswada.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo pia limejitokeza kwa Waheshimiwa Wawakilishi ni lile lilioko katika kifungu cha 4(b) na 4(c) katika ukurasa wa 129 wa mswada. Waheshimiwa wafuatao walilizungumza sana:-

Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Said Ali Mbarouk. Hao ndio wengi waliochangia suala la Bodi ya Sensa kuwa na uwezo wa kukagua kanda za *video* na kadhalika. Pia yalitajwa maeneo kama Tamasha la *ZIFF*, *Busara Promotion* kwamba maeneo haya ndio kanda zao na michezo yao na filamu zingepaswa zikaguliwe zaidi. Nakubaliana na mawazo yaliyotolewa.

Suala la uwekaji wa filamu katika vyombo vya usafiri Mhe. Bi. Raya kazungumza kwa hamasa sana lakini kwa hoja nzito. Ametoa mfano nini kimetokea wakati kanda fulani inaoneshwa katika meli. Nasema tunakubali mawazo yaliyotolewa na bodi itajitahidi kufanya hayo mliotuelekeza na kutushauri. Lakini tumeyasikia vizuri sana maelezo ya Mhe. Raya Suleiman na hili nilitaka nijikite katika kulitolea maelezo lakini sidhani kama nitalitolea maelezo vizuri zaidi kuliko alivyolitolea maelezo Mhe. Bi. Raya.

Washairi wa lugha ya Kiarabu wamesema ifuatavyo: haya ni mashairi sio hadithi ya Mtume (*SAW*) wala sio aya ya *Kur-ani* ni mashairi. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti,

wamesema: ”*Al-elmu fil swighar kaanakshi fil hajjar”,* maana yake nini? Maana yake ni kwamba elimu ya utotoni ni sawa sawa na nakshi iliyochongwa katika jiwe na huwezi kuifuta na ukitaka kuifuta ufanye kazi kweli. Naelekezwa namna ya kuifuta lakini bado nasema ufanye kazi kweli si rahisi.

Mhe. Bi Raya amesisitiza sana kwamba bodi peke yake, wizara peke yake haitaweza kabisa kuyamaliza yale mnayotuagiza tuyafanye, haitaweza. Bodi, sheria hizi zitakuwa rahisi kuzitekeleza na kufanya kazi zake kama mafunzo ya utotoni katika familia yatafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Bi Raya ametoa mifano mizuri sana na akasema sisi familia tubebe mzigo mkubwa. Mimi nasema alivyosema mheshimiwa ni sahihi na hapa mheshimiwa ukiniruhusu nitasema maneno aliyoyasema Mwenyezi Mungu kutilia mkazo hili. Mwenyezi Mungu amesema: ”*Walataziru waziratun wizra ukhuraa, Wamakunna muadhibina hatta nabaatha Rasula”*. Maana yake nini? Kila mmoja atabeba mzigo wake hakuna atakayebeba mzigo wa mwenziwe, lakini adhabu za Mwenyezi Mungu hazitatoka au hazikutoka mpaka Mitume imeteremshwa. Sasa baada ya kuteremshwa Mitume imetuasa na imetuelekeza tufanye nini, tulioelekezwa ni sisi. Kwa Mtume Muhammad (*SAW*) sisi sote na hususan Waislamu tunatakiwa kama alivyosema Mhe. Raya Suleiman Hamad tuwalee vizuri watoto wetu, kuna mifano mingi na sitaki kupoteza muda

Mhe. Mwenyekiti , kama mfano wa baba kuchukua jukumu la nyumba , hilo ni kweli kabisa “*Alrijalu kawamuna alanisai* ” sio katika kudhulumu haki zake Yule mwanamke hapana kumsimamia kumuongoza, na tulobahatika kuhudhuria ndoa za kiislamu tunamskia muozeshaji alivyotwambia wanaume kwamba ‘’ kuanzia leo mama huyu anatoka katika jukumu la wazazi wake wewe mume sasa utabeba jukumu la kumuelimisha huyu na kumfundisha kufanya mema pamoja na kutimiza sala tano kwa wakati wake “ wale waozeshaji wazuri sana huwa wanafanya hivyo”.

Mhe. Raya Suleiman Hamad ametuhimiza leo kwamba sisi wanaume tuna jukumu kubwa tusiwaachie wazazi wa kike peke yao, wakati wazazi wa kike wamsimamie mwanamke na wazazi wa kiume wamsimamie mtoto wa kiume. Naunga mkono kwa asilimia mia moja mawazo ya Mhe. Raya Suleiman Hamad kwa sababu yameungwa mkono au yametokana na aya za quran na ni maelezo ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo , wale wote ni wengi sana wamezungumza kwamba Bodi hii itakua na kazi kubwa na wengine wakadiriki kusema kwamba hivyo Bodi hii itaweza kufanya kazi zake waliuliza. Majibu ya hayo mimi nasema Bodi hii kweli itakua na kazi kubwa . Lakini kufanya kazi zake itaweza, mimi nasema itaweza kwa ile lugha aliyoitumia Mhe. Zakia Omar Juma kwa kumnukuu Rais Barack Obama na mimi niitumie “*Yes we can if you work together”* ndio tunaweza kama tukifanya kazi kwa pamoja.

Hili ni suala nashukuru sana kwa namna ulivyochangia waraka huu au mswada huu haujachangiwa kwa vionjo wala bughudha. Kila aliechangia mswada huu alikua makini sana katika kuukosoa na kuelekeza. Nashuruku sana kwa sababu mswada huu umetugusa

sote, wizara, waziri, Waheshimiwa pia umetugusa zaid kwa sababu kuna watu huko nyuma tunawaongoza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ubora wa karatasi limechangiwa na watu wengi au rangi ya karatasi. Mhe. Salmin Awadh Salmin ndie alieanza, Mhe. Ali Abdalla Ali ameligusia hilo, Mhe. Zakia Omar Juma nay eye pia ameligusia hilo. Jawabu lake ni rahisi. Ni kweli kabsa *observation* ilikuwa sahihi na tunabeba mzigo huu sitaki kusema kosa la Kiwanda cha uchapishaji wala sitaki kusema kosa la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nasema tunabeba mzigo huu na "*inshaallah*" tunajirekebisha na hili halitotokea tena .

Mhe. Mwenyekiti, suala la sita lililozungumzwa na watu wengi, lakini hapa nimeghafilika kunukuu yake majina. Nitakapolizungumza wenyewe watajijua. Mhe. Naibu Waziri wangu amelitolea ufafanuzi. Chuo cha Sanaa. Hili kwa kweli, liko katika mioyo yetu toka tulipoingia katika wizara hii hatujafanikiwa lakini nia ipo na maeneo mawili mazuri sana yameshachaguliwa tutakapopata nyenzo maamuzi makubwa ya serikali tutaanzisha Chuo hiki. Tuliona kwanza tushughulikie uanzishaji wa Chuo cha Habari. Waheshimiwa tutakapopata nyenzo maamuzi makubwa ya serikali tutaanzisha Chuo hiki. Tuliona kwanza tushughulikie uamuzi wa Chuo cha Habari. Waheshimiwa mlizungumzia sana na kila linapozungumzwa neno muhimu hapa Baraza sisi sote mawaziri huwa tunaliangalia kwa umakini sana. Suala la kuanzishwa Chuo sote mawaziri huwa tunaliangalia kwa umakini sana. Suala la kuanzishwa Chuo cha Habari mlilizungumza sana na pengine muda si mrefu tutakuja kukupeni taarifa rasmi kwamba hatma ya kuanzisha chuo hicho sasa imeshapatikana.

Ruhusa ya awali ya kuanzisha ipo lakini tunamalizia suala la masomo na kumchagua msimamizi wa Chuo hicho pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo au wa Kamati ya Baraza la Chuo hicho pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo au wa kamati ya Baraza la chuo, yakimalizika hapo nadhani tutakuwa tumeshafikia kukamilisha mahitaji yote ya chuo, na nataka nikwambie kwamba chuo hiki kimepata msaada mzuri sana kutoka *UNESCO* wa vifaa vya kileo na hata yale mazoezi watakayofundishwa mambo ya bahari na kadhali sasa hawatalazimika tena kwenda redio au kwenye *television* vifaa vyake vitakuwepo ndani ya chuo.

Kwa hivyo, ni chuo cha kisasa ingawa pale kilipo bado haparidhishi sana. Lakini na SUZA nayo ilipo hairidhishi lakini tumeshatoa wahitimu mara nne. Kwa hivyo, bado tunapo pahali pazuri pa kuanzia na *inshaallah* huko mbele tutapata pazuri zaidi. Kwa hivyo, hoja ya Chuo cha Sanaa ni hoja nzito tumeipokea, tunayo na tutaendelea kuifikiria na kuitekeleza. Haya yalikuwa yale ya jumla.

Sasa ningependa niende kwa mtu mmoja mmoja tena kwa haraka haraka kwa sababu kuna wachangiaji wamenisaidia sana kama Mhe. Raya Suleiman na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi ambae alikuwa jana akinikaimu na Mhe. Naibu Waziri wangu na yeye amenisaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, michango yake namshukuru sana mizito mizuri na imeelekeza umefafanua na imeboresha katika baadhi ya maeneo kama kamati ilivyofanya alipokuwa anaiongoza wakati wa kujadili mswada.

Mhe. Waziri Kivuli nampongeza sana waraka wake ulijikita zaidi katika kuelekeza na kuboresha. Safari hii haikujikita katika kulaumu na kuwa na wasi wasi hili linawezakana na hili haliwezekani hapana. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye mwenyewe ni mwanahabari na mwanautamaduni. Mhe. Mwenyekiti, niruhusu nimpongeze Mhe. Waziri Kivuli kwa waraka wake. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada wachangiaji hao wa kawaida ambao huchangiwa kwa kusoma nyaraka zao, lakini akafatiwa Mhe. Ali Abdalla Ali. Nimeshatoa tafsiri ya Mazinagombwe alitaka nimpe tafsiri za nyumba za burudani na akasema hivi ule ukumbi wa Salama tunaweza kuita kwamba ni ukumbi wa burudani.

Kwa kweli, ni sahihi ni nyumba ya burudani. Akataka majumba ya sinema ingawa wachangiaji mmoja alisema hayo majumba ya sinema hivi sasa kwanza hayapo tena. Lakini yangekuwepo basi bad hayo hata kama ni ya ndani lakini bado ni majumba ya burudani na majumba haya si lazima yawe barabarani lakini watu wakizidi watatu, wane, watano ambao si watu wa ile familia ni watu wa kawaida wameingia wametozwa pesa wanaangalia basi wameingia katika nyumba ya burudani.

Suala la sifa za Mwenyekiti, nimeshalitoa ufafanuzi. Mheshimiwa alikuwa na wasi wasi kwamba makosa na adhabu zake zimezungumzwa kijumla jumla. Nataka nimuelezee kwamba hayakuzungumzwa kijumla na makosa yako mengi katika sheria huwezi kulitaja moja moja. Lakini katika kanuni yatatajwa yale ambayo yamekusudiwa. Lakini kwenye sheria tumesema tumetoa rangi ya adhabu ukisema isiyozidi laki tano ndio mswada ulivyosema. Maana yake unaweza ukamtoza laki mbili, moja au elfu sita shilingi moja kutokana na uzito wa lile kosa. Kwa hivyo, hapa hatukuweka jumla tumeweka nafasi kubwa ya jaji apime kosa lenyewe uzito wake na adhabu yenyewe inafaa kwa kosa lipi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipengele hiki cha makosa tumeelezea kwamba hili kosa litakapothibiti na kosa lolote linathibitishwa na jaji bodi hii itakuwa inatafuta kosa kwa mujibu wa kanuni na sheria. Lakini pale kosa limepatikana hii bodi itakayotoza faini bila shaka kosa lile litapelekwa mahakamani.

Mhe. Salmin Awadh Salmin mengi aliyoyazungumza nimeyatolea ufafanuzi hasa zile tafsiri. Alitoa ushauri mmoja mzuri tutakapounda Bodi basi tuangalie uwezekano wa kushirikisha *NGO* katika ule utamaduni tulioujenga sasa hivi wa *Puplic Private partnership* yaani (*PPP*). Ushauri tunachukuwa na tunaufanyia kazi.

Alishauri marekebisho ya kifungu cha 7 na kifungu cha 8. Vifungu hivi nineona akipenda tuliondoe. Tunaukubali ushauri huo na tunafanya kazi. Namshukuru sana Mhe. Salmin Awadh Salmin alipokuwa anatoa utangulizi ambapo alichukuwa muda mrefu kidogo alisema mengi yale ambayo Mhe. Raya Suleiman Hamad alizungumza nayo ni kwamba Bodi hii itakuwa na kazi nzito ngumu na haitawezekana peke yake kutekeleza mambo

yote haya. Kwa hivyo, nakubaliana kabisa ni yale yale niliyoyazungumza mimi kwamba lazima tushirikiane.

Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla) aliuliza tunaelekea wapi suala la kikundi cha sanaa cha taifa kupotosha ngoma zetu za kiasili. Bodi hii sasa hivi pamoja na kikundi hiki kiko katika wizara yangu ni kikundi chetu cha Taifa. Bodi hii sasa hivi ikipata meno makali zaidi itahakikisha kwamba hata nyumba zetu zinakaa sawa kwanza hata kabla hatujaanza kuzihukumu nyumba za wenzetu kwa hivyo, "kila Ngoma itapigwa kwa mdundo wake na itachezwa kwa madaha yake".

Vyombo vya habari vinapotosha maadili ya Mzanzibari katika utumiaji wa lugha na Sanaa, tutajitahidi hilo kulirekebisha Mheshimiwa alieleza yale yaliyoelezwa na wengi kuwa sasa hivi kuna mitandao ni karne mpya ya bodi hivi kweli itaweza kuzuia mambo ya *internet* na akashauri bodi izishauri taasisi za Utalii kuhakikisha maadili ya Mzanzibari katika kivazi kiangaliwe uzuri na watalii wajikite katika kuyapenda maadili yetu kuliko kutuletea yao.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kutokana na hali yetu ya utandawazi sasa hivi haitawezekana hata siku moja kuzuia mambo haya kabisa yasifanyike kwa mfano inaweza kuzipitia filamu, nyimbo, michezo ya kuigiza na kadhalika. Lakini Bodi hata kama pametoka mawazo hapa na hili nataka litolewe ufafanuzi kabisa bodi isiishie katika mambo ya hadhara tu. Bodi iweze kuingia na mambo ya ndani. Mhe. Mwenyekiti, niliambiwa maana walipochangia nilikuwa sipo lakini niliambiwa kuwa Mhe. Haji Faki Shaali alisema kama kifungu cha Katiba kinachomzuia mtu kuingilia mambo ya mwenzake.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha Katiba namba 5 kifungu kidogo namba 1 kichwa cha maneno cha pembeni kinasema " Haki ya faragha ya mtu na usalama wake" sasa Bodi haitaweza kuingia ndani ya nyumba kwenda kuangalia filamu zile ambazo tumeshauriwa tuzifanyie kazi tuziondoshe tuzipige marufuku. Kupiga marufuku filamu za *X* ni suala moja na tutazipiga marufuku kweli kweli na zikioneshwa hadharani aliehusika ataingia mashakani hilo tunaweza kufanya.

Baada ya hapo si dhani kama tunaweza kufanya zaidi kwa sababu filamu za *X* wengine wanaita filamu ya Kibuluu inatoka nje inapita *Custom* imefichwa na pengine watu wa *custom* hawakuiona anaingia katika nyumba ya mtu bila shaka katika nyumba kama familia kuna baba, mama na watoto. Kwa kiasi gani baba atairuhusu filamu hiyo ioneshwe katika nyumba yake na watoto waiangalie ndio lile jukumu lake nililosema kila mmoja atabeba mzigo wake. Mhe. Raya Suleiman amelizungumza sana hilo na sitaki niliendeleze.

Sasa wale waliochangia na kusema kwamba Bodi ya Sensa isiishie kwenye maonesho ya dhazara tu lakini iingie mpaka maonesho ya ndani. Hili kwa kweli kwa mtazamo wowote litakuwa ni gumu na uvunjaji wa kifungu cha Katiba ya "haki ya faragha ya mtu". Kwa hivyo, hivyo naomba hili tuliangalie kwa mtizamo huo. Mhe. Abdalla Juma Muakilishi wa Jimbo la Chonga amezungumza mengi lakini mambo matatu ameyatilia mkazo.

Kwanza, ni kuporomoka kwa silka za Mzanzibari. Ingawa hili liko katika sekta nyengine lakini limezungumzwa sana na nitalitolea jawabu. Lakini kwa ku-*save* wakati Mhe. Raya Suleiman amelizungumzia vizuri sana. Nani anachangia kuporomoka kwa sifa ya Mzanzibari? Kama mtoto wa kiume amefunzwa amefunzika sio rahisi kuvaa ile surali ukanda wake uko mapajani. Hatua aliyoizungumza Mhe. Raya Suleiman kama hatua ile ndio ingechukuwa na baadhi ya wazazi wengi na hasa wanaume mtindo huu mpya usingeendelea. Lakini sijui kwa nini kivazi hiki kinatoka nje kinaingia ndani tunakitizama na tunakistajabia. Lakini hatukikemei. Mhe. Abdalla Juma alishauri jamii ielimishwe katika kulinda maadili yetu.

Kwa upande Bodi itafanya hivyo kwa kutumia vyombo vyake vya habari na yenyewe bodi itavitumia vyombo vya habari katika kujisahihisha vyenyewe kwanza. Halafu itavitumia katika kuelimisha. Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, kuna usemi wa Kizungu unaosema *Education begins at home* maan yake Bodi itasaidia lakini yule ambaye alipata mafunzo mazuri nyumbani itakuwa rahisi kufundishwa, kuliko yule ambae hakupata aliachiwa huru kuangalia hizo filamu na kadhalika si rahisi kumgeuza na kumfundisha.

Mheshimiwa alishauri Bodi ifanye ukaguzi wa kina wa hizi kanda zinazouzwa madukani, hilo linawezekana kwa asilimia mia moja lakini linawezekana. Mhe. Ame Mati Wadi Mwakilishi wa Matemwe. Kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana ni mara chache sana anapochangia bila ya kunukuu kanuni au kunukuu katiba na wakati mwengine ana kionjo chake anasema nanukuu kifungu cha 22 japo kwa kudodosa.

Sasa katika mchango wake alinukuu baadhi ya vifungu vya Katiba na zaidi ya hapo alitaka apatiwe ufafanuzi zaidi wa juu ya vinyago vinavyo polekwa katika eneo la utalii. Nasema kuna vinyago vinavyoshajihisha mwafrika mwanamme lakini hakuwa muazi sana na tulimfahamu kwasababu maneno mengine “kunga” hayazungumzwi hadharani.

Lakini alipozungumza kiwango cha mwanamme cha muafrika kinatengenezwa vibaya nilimfahamu. Viko vyengine hata vya mwanamke vinatengenezwa katika hali hiyo hiyo ambayo havitizamiki. Lakini hali hiyo katika jukumu ambalo linatekelezeka ni bodi kwenda kufanya *survey* katika maduka ya utalii na kuvipiga marufuku vinyago hivyo mara moja, hilo linatekelezeka na nahidi Baraza hili tutalifanyia kazi kwa nguvu zote.

Pia alishauri neno sensa na filamu yapatiwe maneno mbadala katika lugha ya Kiswahili. Tafsiri ya meneno nimeshaitoa, lakini bado leo nadhani nikienda Nungwi au Chokochoko au Kijiji chochote cha Unguja au Pemba ukimwambia mtu habari ya sensa basi anajua maana yake nini kwa hiyo, nini neno lililo toholewa ambalo kwa kiasi kikubwa linakabiliana na lina fahamika. Lakini tutatafuta kiswahili tafsiri fasaha ambacho kitaondosha neon hili ili na madhali neon hilo lipo basi tutalitumia.

Kuna Mjumbe alieuliza matangazo mnayozungumza na mabango ya biashara yatafanyiwa sense vipi. Mhe. Ame Mati Wadi alisististiza matangazo hayo yakaguliwe vipi maana yake nini. Kuna Mjumbe mmoja alipokuja hapa alizungumza. Siku moja katika semina moja hapa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi alizungumza suala hilo.

Akawaambia *ZANTEL* kama mnabandika matangazo kuwashawishi kina mama wanunue simu basi yule mama mliemueka pale kwenye tangazo lile hana silka ya Uzanzibari. Mtuletee matangazo ya mama akijitanda kanga juu na chini vizuri pengine kapaka hina, hizo ndio silka za mwanamke wa Kizanzibari.

Kwa kweli, hayo ndiyo tuliyoyakusudia kuyafanyia uhakiki yaani kuyafanya yawe ya uhakika matangazo kuanzia sasa yote yanayobandikwa mabarabarani, yaani hapo yako hadharani yakubalike katika silka ya Kizanzibari na kiutamaduni wa Kizanzibari.

Mhe. Rashid Seif Suleiman alitaka kujua kwa nini muundo wa Bodi uwe na Wajumbe 6,8,10 badala ya kuwa na 5,7,9. Kwa lugha nyengine kwa nini wawe *even* wasiwe *odd*. Pia akawa na wasi wasi ambao hasa ulikuja pale wakati wa kupiga kura kupatikana ile idadi kubwa iliyoshinda idadi ndogo. Nasema hili tutalichukua, lakini namhakikishia kwamba kwa sababu Mwenyekiti atakuwa na kura ya ziada huo wasi wasi itakuwa haupo. Kwa hiyo, tutaziangalia pande zote mbili za ushauri na tutatizama tukubaliane kwamba lile lililokuwa zuri tutalichukua.

Alishauri kwamba bodi ipatiwe vyombo vya kutendea kazi. Vipo vyombo ambavyo *immediately* vinaweza kupatikana, lakini kuna vyombo havitaweza kupatikana kwa haraka na kwa hivyo bodi bado itakuwa na uchache wa vyombo vya kufanyia kazi kwa uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa asilimia mia moja.

Suala lile la maduka ya kanda na video tumeshalitolea ufafanuzi na narejea tena kusema kwamba hilo ni rahisi kabisa kutekelezwa. Lile neno sensa litafanyika kuangalia maduka yote, idadi za kanda na kadhalika, na kuzifanyia uhakiki zile kanda ambazo haziendani na maadili tutazizuia. Wale watakaopenya na tukawajua kwamba wamepenya tutawashika na kuwapeleka katika vyombo vya sheria.

Mhe. Said Ali Mbarouk mchango wake mwingi ulikuwa ushauri. Alishauri madhumuni ya waraka iwe ni kufufua na kuhifadhi mila na desturi za utamaduni wetu, badala ya kulinda mmong’onyoko. Nadhani ni mtazamo wa tafsiri. Mmong’onyoko upo na Kiswahili ukisema kulinda mmong’onyoko basi Mhe. Said amekuwa sahihi kwa sababu unaulinda huo ubaya uliopo usitoweke. Lengo si hilo, lengo ni kuulinda pasitokee mmong’onyoko. Hivyo ulivyotwambia kwamba kulinda utamaduni, basi tunalinda mmong’onyoko usitokee.

Ushauri wa kuweka daraja ya viwango katika kanda za filam katika kuzifanyia uhakiki tunauchukua, tunaukubali na tunaufanyia kazi. Mhe. Said Ali Mbarouk kama ulimsikia Mhe. Raya Suleiman Hamad, basi alikuwa anakuunga mkono katika yale uliyoyasema kutoa wito kwa wazazi na jamii kusaidiana na serikali katika kuipa nguvu bodi hii na kuweza kutekeleza yale tunayokusudia.

Alishauri nafasi ya uteuzi wa Afisa Mtendaji itangazwe, badala ya kuteuliwa na Waziri iwe ateuliwe na Rais. Labda nitoe ufafanuzi kidogo. Tumezoea kawaida kuwa na ama Mkurugenzi Mtendaji au Katibu Mtendaji kwa vile vyombo vilivyokuwa vizito au vikubwa. Huyu kwa makusudi tumemwita Afisa Mtendaji kwa sababu kazi zake ziko

zaidi katika utendaji kuliko katika uongozi. Huyu ungeweza kumwita Katibu wa Bodi ukitaka, ndio maana tukamwita Afisa Mtendaji hatukumwita Mkurugenzi Mtendaji au Katibu Mtendaji. Kwa maana hiyo, ndio maana tukasema atateuliwa na Waziri na Rais tumwache amteue Mwenyekiti.

Suala la kumtangaza tunalipokea kwa sababu ya kuwa ni mtendaji pengine atahitaji awe na fani na *qualification* maalum. Kwa hivyo, tukitangaza tutapata wigo mpana zaidi wa kuchagua yule aliye bora. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa kutangaza tunauchukua.

Mheshimiwa alitaka tutoe ufafanuzi kuhusu kifungu cha 7 (1) (b) kinachozungumzia kigezo cha tabia mbaya. Kigezo cha tabia mbaya iwe katika bodi, iwe katika jamii, kigezo chake aghlabu huwa ni kitendo ambacho ama kinakera, kinaudhi jamii, kinakwenda kinyume na maadili ya jamii, kinyume na kanuni, kinyume na sheria na kadhalika. Kwa hivyo, tafsiri yake ni pana kidogo, lakini kwa ufupi tabia mbaya maana yake ni tabia ambayo jamii hawaipendi. Kulewa hadharani ukapita ukifanya haja kubwa na ndogo ovyo ni tabia mbaya, kupita ukitukana watu ovyo ni tabia mbaya, hata kama una uhuru wa kufanya utakavyo, lakini kuvua nguo hadharani ni tabia mbaya. Kwa mfano unakuja katika mikutano ya bodi umelewa badala ya kujadili unagombana, hizo ni miongoni mwa tabia mbaya.

Michango mingine ya Mheshimiwa tumeshaijibu tulipokuwa tunajibu michango ya jumla. Tumelipokea wazo la kuitaka Wizara ya Fedha iiongezee *ceiling* Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ili bodi iweze kutekeleza kazi zake vizuri. Mimi sidhani kama ushauri huo nitaukataa, nauunga mkono bajeti ijayo tutakapojadili wizara hii Mheshimiwa nitakuomba sana nikukumbushe uje unisaidie katika kutetea suala hili.

Mhe. Haji Faki Shaali ni Mjumbe wa Kamati amechangia sana kwenye kamati, ametuelezea mengi na hapa ameongezea yale ambayo kwenye kamati ama aliyasahau au pengine aliona aongezee, ili tutakapoutayarisha mswada huu uwe unaiva vizuri zaidi.

Alichangia sana katika suala la ukiukwaji wa maadili. Kama alivyosema Mhe. Raya Suleiman Hamad, kwamba suala hili si la bodi peke yake, lakini limehusu serikali, limehusu bodi, limehusu jamii na wazazi kwa jumla, nakubaliana nae. Alizungumzia kuhusu suala la uoneshaji filam binafsi. Alizungumzia kwamba Zanzibar haina utamaduni wa peke yake. Bahati mbaya sikuwepo, lakini ningekuwepo ningemshangilia sana, hili huwa nalisema sana kwamba huwezi katika ulimwengu wa leo ukajifungia ndani wewe na utamaduni wako na utamaduni wako na wewe. Siku moja niliuliza swali katika mchango fulani. Je, kinamama mko tayari turudi katika zile behdani, turudi katika zile karatasi za masikio yaani tutoboe masikio yawe kama ya Mmasai. Tunakubali hilo?

Mhe. Mwenyekiti, kama tunakumbuka Mzee Ali Hassan Mwinyi alisema kwamba kila zama huwa na kitabu chake. La msingi kwa sababu ulimwengu mzima sasa hivi unazungumza *cultural diversity* na tunahudhuria katika masemina, maana yake kuna mchanganyiko sasa hivi wa *culture*. Kwa hivyo, kwanza tunachotakiwa tuige kilichokuwa kizuri, lakini la pili tuifanye ile *culture* yetu wenzetu waiige, tusiwe tunaiga sisi tu, tukifanya hivyo tutakuwa tumefanya jambo la maana sana. Lakini tukisema

tunaziacha tamaduni za wenzetu tu moja kwa moja na ilhali ziko zinakuja tunaziona *live* kwenye matelevisheni, tunaziona kwenye watalii, haiwezekani.

Kama tunaweza si kumtungia sheria, maana pametoka hoja hapa labda mtalii tumtungie sheria avae kanzu ndefu na kadhalika hapana. Sasa hivi wapo wazungu wanavaa kanzu ndefu, wapo wazungu wanasuka nywele, wapo wazungu wanapaka hina. Hizo ndio kazi zetu za kuchukua tamaduni zetu kuziuza kwa wenzetu wakija waige zetu vile vile. Tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidiana sana na bodi hii na naomba sana tufanye hivyo. Mhe. Haji Faki Shaali nimehadithiwa sikuwepo lakini nakushukuru sana kwa mchango wako huo.

Pia alishauri tutakapoteua bodi yetu hii uteuzi uwe wa mchanganyiko. Tumeshaanza kuchanganya tokea sasa hivi hapa. Ninahakika panapo uhai wangu mimi na Mhe. Raya Suleiman Hamad, maadam mimi ndio ninaeteua na wenzangu wanaonisaidia wapo wamenisikia na wametusikia, mchanganyiko mmoja tumeshaupata na huu unatokana na mchango wake hautokani na Mhe. Raya. Tukilazimika kumuongeza mwanamke mwengine kutoka kwenye Baraza hili tunae tumeshamtupia jicho hatumtaji sasa hivi. Suala la *NGO* tumesema tutalifuatilia. Kwa hivyo Mhe. Haji Faki Shaali ushauri wako mzuri tunaupokea.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis amependekeza bodi hii tuiite Bodi ya Uhakiki badala ya kuiita Bodi ya Sensa. Mhe. Mwenyekiti, ukisoma jina la mswada huu basi ni refu kidogo ingawa ni fupi kuliko lile la mwanzo. Kwa hivyo si Bodi ya Uhakiki wala si Bodi ya Sensa peke yake imeeleza pale penye jina. Warka kidogo upo mbali na sina muda wa kupoteza, lakini ukiutazama lile jina utalikuta. Ushauri wako tumeupokea, lakini naomba tubakie na jina hili hili kama lilivyo katika warka ule.

Uhakiki ufanywe kwa filam zote za ndani na nje. Ndivyo tulivyokusudia kwa filam ya nje ikiingia ndani. Maana hatuwezi kwenda Marekani kufanya uhakiki wa filam zinazooneshwa huko. Lakini filam ya Marekani ikiingia ndani humu, basi tufanye uhakiki, hilo ni jukumu la bodi. Shauri hili lilitolewa na watu kiasi watatu, wawili nilipokuwepo niliwasikia. Kanda zitakazohakikiwa ziwekewe alama maalum yaani ziwe *sealed*. Hilo wazo halipingiki ni sahihi kabisa, tutautafuta utaalam huo, ili tusihakiki na baadae tukahakikiwa, tuhakiki kwa maana ya kuhakiki hasa ili kilicho kibaya tunakitoa.

Mhe. Ali Denge Makame ushauri wako tumeupokea. Tuwe makini katika vyombo vyetu vya habari kuonesha filam. Wajumbe wa bodi wawemo watu mashuhuri tumepokea na tutalifuatilia suala hili.

Mhe. Zakiya Omar Juma kwa sababu ya muda naomba ukubali na wewe unajua kwamba nimethamini mchango wako wote ulioutoa na tutaufanyia kazi. Mchango wa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kama nilivyosema, ulisaidia sana kutoa ufafanuzi wa hapa na pale katika yale maswali yaliyoulizwa. Mchango wa Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak uliweka mkazo sana katika kutunza maadili, na kutuasa kwamba tusiposimama kidete katika kuyalinda maadili yetu, mmong'nyoko mkubwa utatokea. Akatutahadharisha kwamba hali iliopo sasa ya ukimwi nayo inachangiwa kutokana na

yale machafu tunayoyafanya. Mheshimiwa nakubalina na wewe mia juu ya mia. Kuhusu mavazi nimeshayatolea mfano tuwalazimishe vijana wetu wavae vizuri majumbani mwetu. Michezo ya kuigiza umeitolea mifano tunapokea ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, wa mwisho ni Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambaye ame-*react* katika hoja zake na mimi nakubaliana nae kabisa na muono wake. Mhe. Mwenyekiti, kama utaniruhusu tena nitoe shukurani za pekee. Katika kipindi chote ambacho Mhe. Raya Suleiman Hamad yupo hapa Barazani nimekuwa nikifuatilia sana michango yake lakini ya leo imefurutu ada, si kwa maana mbaya, lakini kwa kutuelimisha na kutukumbusha majukumu yetu kinababa na kinamama majumbani mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filam za Maonesho**

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA BARAZA ZIMA

**Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filam na Sanaa za Maonesho**

Kifungu cha 1 -

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilipokuwa nazungumza kuhusu kifungu hichi naona Mhe. Waziri hakulizungumza. Naomba nipate ufafanuzi. Nilisema kwamba hili jina sensa kweli limetoholewa kutoka Kiingereza kwa maana ya *censorship*. Lakini kwa bahati mbaya kwamba Kiswahili hichi hichi tunatumia kuhesabu idadi ya watu. Vipo vitabu vimeandikwa hasa jina hili na *spelling* hizi hizi. Sasa sisi tumekuwa tunatoa ushauri kwamba hakuna jina jengine linaloweza kutumika, ili kuondoa ule utata ambao ungejitokeza kwa jina moja hili hili kutumika kwa maana ya hesabu ya watu, na wakati huo huo linatumika kwa maana ya kuchunguza na kuhakiki. Naomba ufafanuzi.

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, huu ushauri si mbaya, lakini nataka nimkumbushe Mhe. Rashid kwamba ni jambo la kawaida neno moja kutumika kwa maana ya zaidi ya moja. Kwa hivyo, sensa

haitumiki peke yake kwamba ni maana ya hesabu ya watu, kufanya kitu sensa maana yake ni kukihesabu. Yumkini kwamba watu, kanda za video, visahani vya santuri na kadhalika. Kwa hivyo hapa kilichokusudiwa tumelitohoa neno hili kwa kukusudia kwamba patafanyiwa hesabu, utafiti, zitachunguzwa kanda na kadhalika. Kwa hivyo, jina hili la sheria hii litajulikana kama Sheria ya Sensa ya Filam na Sanaa za Maonesho. Hapa *specifically* ni Sensa ya Filam na Sanaa za Maonesho. Ikiwa ni lazima sana kubadilisha, basi tutafikiria kutafuta jina lililokuwa bora zaidi, lakini naona jina hili bado halijaharibu mantiki. Sensa ya filam sio sensa ya watu.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sheria wenyewe hasa ni wale walengwa wananchi wengi tunaoifahamu ndio sisi tuna wasi wasi huo. Ikiwa Mhe. Waziri anatuhakikishia kwamba hakutokuwa na mashaka ya ufahamu wa watu basi naomba tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu cha 1 | - | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| Kifungu cha 2 | - | Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 3 | - | Kuanzishwa kwa Bodi. |
| Kifungu cha 4 | - | Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 5 | - | Muundo wa Bodi. |
| Kifungu cha 6 | - | Muda wa Wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 7 | - | Kusimamishwa au Kusitishwa kwa Mjumbe pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 8 | - | Mikutano ya Bodi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 9 | - | Uwezo wa Bodi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 10 | - | Uteuzi na Uundaji wa Kamati. |
| Kifungu cha 11 | - | Mualiko. |
| Kifungu cha 12 | - | Malipo ya Wajumbe wa Bodi. |
| Kifungu cha 13 | - | Uteuzi wa Afisa Mtendaji pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 14 | - | Majukumu ya Afisa Mtendaji pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 15 | - | Fedha za Bodi. |
| Kifungu cha 16 | - | Majukumu ya Afisa Mtendaji juu ya Fedha pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 17 | - | Mahesabu na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 18 | - | Ripoti ya Mwaka pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 19 | - | Utaratibu pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 20 | - | Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 21 | - | Dhamana kwa Bodi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 22 | - | Kanuni pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu cha 23 | - | Mawasiliano na Bodi. |
| Kifungu cha 24 | - | Kufutwa kwa Kifungu cha 18 hadi 39 vya Sheria Nam. 6 ya Mwaka 1983. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu

baada ya kifungu na kuukubali bila ya mabadiliko yoyote pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali mswada huu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filam na Sanaa za Maonesho pamoja na marekebisho yake**

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mweneyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Sensa ya Filam na Sanaa za Maonesho usomwe kwa mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada ya Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya pili na kupitishwa)*

**TAARIFA**

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa vile shughuli zote zilizoorodheshwa leo katika *order paper* zimekamilika, basi naomba kwa ruhusa yako tuliahirishe Baraza hili mpaka kesho saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 23/01/2009 saa 3:00 asubuhi)*